

**AMORIM AKUBALI KUHAMIA UNITED**

UKURASA 21

**VIPIMO** DNA vyamaliza utata maiti yenye mzozo

UKURASA 2

**WAZIRI** ataja mafanikio 10 ya uwekezaji wa DP World

UKURASA 4



**WADAIWA** kutelekeza familia zao kisa ulevi

UKURASA 15

epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Jumamosi Novemba 2, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 085 ... 0581848

www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
epaper.ippmedia.com

LIKE & FO... 0745 700 710 nipash... ...eTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital



## Jenerali Mstaafu Musuguri aagwa kwa heshima Dar

UKURASA 3

Mwili wa Mkuu wa Majeshi mstaafu, Jenerali David Musuguri, ukiwasili katika viwanja vya Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo, Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kuagwa. **Picha ndogo:** Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiwaongoza waombolezaji kutoa heshima za mwisho. **PICHA: OMR**

**BAJETI 2025/26**

# TRL. 55/- KUKUSANYWA

**VIPAUMBELE** vyaanikwa, kimo Uchaguzi Mkuu 2025 .. *Endelea ukurasa wa 2*



Maliki Hashimu

## Mtoto aliyekatwa koo na dada arejeshewa uwezo kuzungumza

UKURASA 3




Skani hapa kutembelea chaneli yetu

**MICHEZO** GAMONDI, TAOUSSI MECHI YA MARAFIKI UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# DNA yamaliza utata maiti yenye mzozo

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MWILI wa mtu aliyedaiwa kuwa Jackson Joseph (29), mkazi wa Kijiji cha Kibosho Kindi, Moshi mkoani Kilimanjaro, aliyefariki dunia Juni 16, mwaka huu, kutokana na majeraha yaliyosababishwa na kipigo kisha kuzikwa na familia yake, majibu ya uchunguzi wa Vinasaba (DNA), yamebaini haukuwa wake.

Kabla ya kuzikwa, mwili huo ulioibua utata, ulikaa chumba cha kuhifadhia maiti cha Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC kwa siku 59 kutokana na familia mbili kuvutana nani mwenye haki ya kuzika.

Jackson kabla ya kupoteza maisha Juni 16, alidaiwa kushambuliwa kwa kipigo Juni 25, huku familia mojawapo ikidai si Jackson aliyefariki dunia bali ni Richard Shoo.

Akizungumza jana nje ya Kituo Kikuu cha Polisi Moshi muda mfupi baada ya kupewa majibu hayo, mama mzazi wa marehemu, Agness Ullomi, alisema amekuwa akifuatilia jambo hilo polisi mara kwa mara ili kuhakikisha anapata haki ya kumzika mtoto wake.

"Ninaipongeza Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Jeshi la Polisi na madaktari kwa kuhakikisha haki inapatikana. Familia tumeamua maziko ya mtoto wangu yatafanyika Novemba 4, mwaka huu, eneo la Msitu wa Tembo, kata ya Arusha Chini, wilaya ya Moshi," alisema.

Mzozo huo, ulisababisha mwili wa Jackson aliyefananishwa na Richard Shoo, kufukuliwa Septemba 4, mwaka huu, na kuhifadhiwa tena KCMC hadi leo.

Bibi wa marehemu, Magreth Fransis, alisema mjukuu wake alifariki dunia kwa kupigwa, akisadikika kuwa mwizi lakini hawakupata taarifa kama familia, jambo lililosababisha familia nyingine kuuchukua mwili na kwenda kuuzika wakidai kuwa ni mtoto wao.

Alisema baada ya kutomwona kwa muda mrefu, walikwenda kutoa taarifa polisi na kuelezwa kuwa yuko kijana aliyeuawa kwa kudaiwa ni mwizi na amezikwa Kibosho Kindi.

Alisema walipofuatilia walibaini ni mtoto wao, ndipo walipoomba mahakamani kibali cha kufukuliwa mwili huo na kufanyiwa uchunguzi wa DNA.

Msemaji wa familia iliyokuwa imeuzika mwili huo awali, Corodias Shoo, alisema wanakwenda kukaa na wazee wa ukoo ili kuona kaburi ambalo lilifukuliwa mwili huo wanalifanya nini kwa sasa kwa sababu walilifunika tu.

Alisema hawajaridhishwa na utaratibu wa uchukuaji wa vipimo vya DNA akidai kuwa marehemu huyo ni mtoto wao aitwaye, Richard Shoo.

"Siamini kama mtoto wetu bado yuko hai kwani tumemtafuta sana maeneo mbalimbali na hana tabia ya kukaa nje muda mrefu bila kufika nyumani.

"Kwa vyovyote vile, mtoto wetu hayuko duniani tena lakini tutaendelea kumtafuta kwa sababu tumeambiwa huyu marehemu si mtoto wetu,"alisema.



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba akiwasilisha mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya serikali kwa mwaka 2025/2026, bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Trl. 55/- kukusanywa mwaka 2025/26

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI inakadiria kukusanya na kutumia Sh. trilioni 55.06 kwa mwaka 2025/26, huku ikitaja maeneo sita mahsusi yatakayopewa kipaumbele ikiwamo kugharamia maandalizi ya Uchaguzi Mkuu mwaka 2025.

Aidha, misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo inakadiriwa kuwa Sh. trilioni 1.02, mikopo nafuu Sh. trilioni 5.6 na mikopo ya kibiashara kutoka vyanzo vya ndani na nje Sh. trilioni 9.4.

Akiwasilisha bungeni jana mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema maeneo mengine yatakayopewa kipaumbele ni uendelezaji wa miundombinu, uimarishaji wa sekta za uzalishaji na huduma za jamii.

Aliyataja maeneo mengine kuwa ni usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi, kuboresha usimamizi na mifumo ya kitaasisi, ili kuimarisha utawala bora na kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa makundi maalum.

Dk. Nchemba alisema kati ya fedha hizo, mapato ya ndani ni Sh. trilioni 38.9 ikilinganishwa na maoteo ya Sh. trilioni 34.6 mwaka 2024/25. Ongezeko hilo limezingatia misingi ya uchumi jumla, mikakati na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na serikali kuimarisha ukusanyaji wa mapato.

Alitaja hatua hizo ni kuhimiza matumizi ya mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), kudhibiti utoaji wa misamaha ya kodi na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji zitakazowezesha uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato.

"Dhamira ya serikali ni kuhakikisha kuwa mapato ya ndani yanaendelea kugharamia kiasi kikubwa kwenye bajeti ya Serikali kisichopungua asilimia 70 ya bajeti yote.

" Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na taasisi nyingine za serikali, itaendelea kutekeleza mkakati wa muda wa kati wa ukusanyaji wa mapato wenye lengo la kuongeza mapato ya ndani na kupunguza utegemezi wa mikopo na misaada katika bajeti," alisema.

Kuhusu matumizi ya fedha hizo, Waziri alisema yanatarajiwa kuwa Sh. trilioni 55.06. kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida yanatarajiwa kuwa Sh. trilioni 38.6 na maendeleo Sh. trilioni 16.4.

**MAELEKEZO 10 MAHSUSI**

Dk. Nchemba alisema mwongozo huo umeainisha maelekezo mbalimbali ambayo maofisa masuuli wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu wakati wa uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mpango na bajeti.

Maelekezo hayo aliyataja kuwa ni pamoja na kuzingatia ukamilishaji wa miradi inayoendelea kabla ya kuibua miradi mipya, kulipa madeni ya miradi inayoendelea au iliyokamilika na mapato yote yanayokusanywa luingizwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Pia alisema mafungu yanaelekezwa kuzingatia matumizi ya Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE) wanapofanya malipo, matumizi sahihi ya mifumo ya kielektroniki ya serikali ya ukusanyaji wa mapato kwa kufanya uhakiki, usuluhishi na ukaguzi wa mifumo mara kwa mara kwenye vituo vyote vya makusanyo, ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato.

"Kutekeleza Mwongozo wa Utaratibu wa Maombi na Utoaji wa Fedha wa mwaka 2021, unaosisitiza kutoingia mikataba bila kuwa na uhakika wa fedha ili kuzuia ulimbikizaji wa madeni.

"pia kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma iliyoweka ukomo wa zabuni zinazoweza kutolewa kwa wasio wazawa ili kuwawezesha wazawa na kuongeza mzunguko wa fedha katika uchumi; pamoja na kuzingatia matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa ununuzi wa umma," alisema.

Dk. Nchemba alisema watendaji wazingatie kutoingia mikataba na wazabuni bila kufuata sheria, taratibu na miongozo ikiwamo sheria za kodi, miradi mipya isiyo na maandalizi ya msingi kama vile malipo ya fidia kupisha mradi au upembuzi yakinifu.

"Kutekeleza mkakati wa taifa wa kuimarisha upatikanaji wa fedha za kigeni ikiwamo kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima ya fedha za kigeni, kuongeza uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa mauzo ya nje, kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, ili kuvutia mitaji kutoka nje ya nchi, na kutoa kipaumbele kwa bidhaa na huduma za ndani," alisema.

Pia alisema kufuatilia kwa karibu utendaji wa mashirika ya umma hususani yale yanayojiendesha kibiashara na kuyaandalia mkakati wa kuyawezesha kujiorodhesha katika soko la hisa, ili kupunguza wajibu wa serikali kudhamini na kugharamia uendeshaji wa mashirika hayo.

Waziri huyo alisema ushirikishaji wa sekta husika katika utekelezaji wa miradi inayohusisha sekta zaidi ya moja kabla, wakati na baada ya utekelezaji na kuzingatia masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi pamoja na masuala ya jamii katika upangaji na utekelezaji wa bajeti ya miradi ya maendeleo.

**UTEKELEZAJI BAJETI**

Alisema katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2024/25, serikali imekusanya Sh. trilioni 11.5 kutoka vyanzo vyote vya ndani na nje. Kati ya fedha hizo, Sh. trilioni 7.9 ni mapato ya ndani, sawa na asilimia 99.4 ya lengo la Sh. trilioni 7.9.

Alisema misaada na mikopo nafuu ilifikia Sh. trilioni 1.37, mikopo ya kibiashara kutoka masoko ya ndani ilifikia Sh. trilioni 1.6 na mikopo ya kibiashara kutoka nje ilifikia Sh. bilioni 593.65.

"Katika utekelezaji wa kipindi hicho, ilitolewa ridhaa ya Sh. trilioni 11.6 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo.

"Ridhaa ya matumizi ya Sh. bilioni 114.20 iligharamiwa kwa mkopo wa muda mfupi kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ambayo yapo ndani ya kiwango kinachokubalika kisheria," alisema.

HABARI KITAIFA



Mtoto aliyejeruhiwa na 'hausigeli' kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali kooni, Maliki Hashimu (6) mkazi wa Goba, akigonga tano na Bingwa Mbobezi wa Upasuaji Shingo na Mkuu wa Idara ya Pua Koo na Maskio (ENT) wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Aslam Nkya, baada ya kuzungumza na waandishi wa habari, hospitalini hapo, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kumalizika kwa matibabu yake yaliyochukua kipindi cha miezi minne. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Mtoto aliyekatwa koo na dada arejeshewa uwezo kuzungumza

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imemrejeshea uwezo wa kuzungumza mtoto Maliki Hashim (6), ambaye aliupoteza baada ya kupata majeraha shingoni yaliyoathiri koo.

Mtoto huyo, mkazi wa Goba, Dar es Salaam, alikumbwa na madhila hayo baada ya kukatwa na kitu chenye ncha kali shingoni, Julai, mwaka huu, na anayedaiwa kuwa 'hausigeli' wao.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alisema mtoto huyo amerejeshewa uwezo wa kuzungumza baada ya kukamilisha matibabu yaliyogharimu Sh. milioni 15 kwa ndani ya miezi minne.

Prof. Janabi alisema matibabu ya mtoto huyo yamefanyika hatua kwa hatua na watalaamu wamejiridhisha kulingana na huduma alizopata.

"Katikati ya Julai, mwaka huu, tulimpokea Maliki hali yake haikuwa nzuri. Kulikuwa na tuhuma dada wa kazi amemkata koo na tulipochunguza, tulibaini alikuwa amekatwa sana koo na lilikuwa karibu linagusa 'voice box' ( kisanduku cha sauti). Hatari yake ilikuwa angeweza kupoteza sauti maisha yake yote.

"Jitihada ya kwanza iliyofanyika ni kuhakikisha mishipa yote imezibwa ili isiendelee kutoa damu na hatua ya pili ni kisanduku cha sauti kisiathirike na mtoto alikuwa amepoteza fahamu.

Alipofikishwa hapa na mama wa Maliki, alikuwa analia muda wote.

"Baada ya upasuaji na siku 25 akiwa ICU (chumba cha uangalizi maalumu) katika saa 48 za kwanza, Rais Samia Suluhu Hassan, alisema gharama zote tumpelekee yeye na hadi leo (jana) zimefikia Sh. milioni 15," alisema.

Prof. Janabi alisema baada ya kumtoa ICU kwa siku 25 walimrudisha wodini ambako alikaa wiki mbili na kutokana na madhara makubwa aliyoyapata, walimtengenezea njia ya koo bandia, kwa ajili ya kupumua na kula chakula.

Alisema walimruhusu kurudi nyumbani awamu ya kwanza akisubiri hatua ya pili, ambayo ndiyo hiyo ya kuzungumza.

"Hatua za kwanza tulifanya na madaktari bingwa wazawa wataalamu wa ENT (sikio, pua na koo). Pia tulishirikisha wenzetu kutoka California, Georgia huko Marekani wamwone, tukamleta mtoto wiki hii na kuingizwa chumba cha upasuaji na leo (jana) tunamruhusu kwa asilimia 100 na hahitaji tena kufanya tiba," alisema.

Alisema hatua hiyo ya tiba na zingine, inatokana na uwekezaji mkubwa ukiwamo wa vifaa unaosaidia kuleta mafanikio chanya, ambapo nyuma matibabu yake yangefanyika nje ya nchi kwa gharama kubwa.

"Mama na mtoto wangekuwa nje ya nchi kwa miezi minne ni gharama kubwa. MNH tutaendelea kutoa tiba bobezi, uwekezaji huu inawasiadia hata wataalamu tulionao kuonesha uwezo wao," alisema.

Mbobezi wa Upasuaji Shingo na Mkuu wa Idara ya ENT Muhimbili. Dk. Aslam Nkya, alisema mtoto huyo ameruhusiwa baada ya kujiridhisha amepona tatizo alilopata. Alisema awali alikaa na kifaa cha bandia kooni kwa miezi miwili kuruhusu upumuaji.

"Tumejiridhisha sasa amepona baada ya wiki hii kuangalia kidonda chake kimepona, tumekaa kwa siku mbili na palepokuwa na kovu tumeparekebisha sasa amepona," alisema bingwa huyo.

"Mtoto alipofikishwa hospitalini alikuwa na jeraha mbele ya shingo, lililoharibu tezi la mbele liitwalo (thyroid gland), baada ya kukatwa katikati na kusababisha mtoto huyo kuvuja damu kwa wingi, kupata maumivu makali sehemu iitwayo (trachea) ambako hewa inatoka kwenye mapafu hupita iweze kwenda kwenye sanduku la sauti, kumwezesha kuhema, kuongea. Kwa hiyo mantiki vyote vimerejeshwa katika hali yake ya kawaida," alisema.

Mama wa mtoto huyo, Shani Charles, alisema alipofika hospitalini hapo awali, alichanganyikiwa na sasa matibabu yamefanikisha mtoto wake kupona.

Alisema anamshukuru Rais Samia kwa kugharamia tiba na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, ambaye alikuwa na mawasiliano nao mara kadhaa kuhakikisha tiba inafanyika.

"Kipekee ninamshukuru Rais Samia, kwa kulipa gharama za matibabu Sh. milioni. 15. Ninawashukuru watoa huduma wote wa hospitali walioshiriki kumuhudumia mpaka hatua aliyofikia leo kuruhusiwa moja kwa moja, jamii ya Watanzania walioguswa na tukio pamoja na vyombo vya habari vilivyofuatilia kwa karibu jambo hili," alisema.

# Jenerali Musuguri aagwa kwa heshima

**Na Restuta James**

MWILI wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Mstaafu, Jenerali David Musuguri, jana uliagwa kwa heshima za kijeshi Dar es Salaam, huku Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiwasihi Watanzania wailinde nchi kwa hali na mali.

Dk. Mpango ambaye aliongoza waombolezaji katika kutoa heshima za mwisho kwenye viwanja vya Jeshi Lugalo jana, alisema Jenerali (mstaafu) Musuguri ameacha alama ya utumishi mwema akiongoza Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwa weledi, hali na mali.

Viongozi wengine waliotoa heshima za mwisho ni pamoja na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob Mkunda na Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Emmanuel Nchimbi.

Wengine ni Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais mstaafu, Jaji Joseph Warioba, na wakuu wa majeshi wastaafu, majenerali (wastaafu) Hagai Mrisho Sarakikya, George Waitara, Davis Mwamunyange na Venance Mabeyo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dk. Mpango alisema Jenerali Msuguri alipopewa jukumu la kuongoza Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), alifanya jitihada kubwa kulijenga na kuliendeleza na kulifanya kuwa moja ya majeshi bora na imara barani Afrika.

"Ndiyo maana jeshi la Idi Amini lilipovamia kipande cha ardhi ya Tanzania, walikipata cha moto. Katika kumuenzi, inatupasa Watanzania wote, askari na raia, kujitoa na hata ikibidi kufa kwa ajili ya kulinda na kutetea uhuru, heshima na maslahi ya nchi yetu," alisema.

Dk. Mpango alitoa rai kwa vijana kuipenda nchi na jeshi, kwa kuwa tayari kuitetea dhidi ya adui.

"Rai yangu hasa kwa vijana, ni kuipenda nchi yetu na jeshi letu kwa moyo wote na kuwa tayari kumlinda mama Tanzania kwa gharama yoyote kama alivyofanya Hayati Jenerali Mstaafu David Musuguri.

"Vivyo hivyo kwa majerali, majenerali, makamanda na wapiganaji mliopewa dhamana ya uongozi katika jeshi letu, hamna budi kuendelea kufuata mfano bora aliotuachia Jenerali mstaafu David Msuguri," alisema.

Jenerali Msuguri ambaye alisafirishwa jana kwenda Butiama atazikwa Jumatatu. Alizaliwa Januari 4, 1920 na kujiunga na jeshi mwaka 1943. Alipanda vyeo na kutunukiwa nishani mbalimbali na kuteuliwa kuwa mkuu wa majeshi.

Alifariki dunia Oktoba 29, katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, Mwanza, alikokuwa akipatiwa matibabu.

## Dk. Mwinyi ahimiza amani, mshikamano kuelekea uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu,**
PEMBA

RAIS wa Zanzibar, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi, amei-kumbusha jamii kuendelea kutunza amani na mshikamano uliopo na kuendelea kujenga maendeleo ya nchi.

Amesisitiza kuitunza amani hasa wakati wa uchaguzi unapokaribia nchini na kuitaka jamii kutotofautiana na kufarakana wakati wa uchaguzi mkuu, hivyo kuwataka kuendelea kuwa kitu kimoja.

Dk. Mwinyi alisema hayo jana Masjid Hudaa, Machomane wilaya ya Chake Chake, Kusini Pemba alipojumuika na waumini wa Dini ya Kiislam kwenye Ibada ya Sala ya Ijumaa.

Kwa mujibu wa taarifa uiliyotolewa na Idara ya Mawasiliano Ikulu, Zanzibar, Dk. Mwinyi alisema nchi inahitaji idumu kwenye amani huku akisisitiza kuwa maendeleo yoyote yanapatikana kutokana na kuwapo kwa amani, umoja na utulivu.

Alisisitiza kuwa bila nchi kuwa na rasilimali ya amani hakutokuwa na jambo lolote litakalofanyika na kufanikiwa.

Katika kutilia mkazo suala la amani na utulivu, Dk. Mwinyi alitolea mfano wa mataifa mengine duniani yaliyo kwenye migogoro na kutokuwa na utulivu kwa nchi zao hali aliyoieleza kuathiri maendeleo ikiwamo uchumi kutetereka.

Akizungumza kwenye ibada ya sala hiyo, Katibu Mtendaji kutoka Ofisi ya Mufti Zanzibar, Sheikh Khalid Ali Mfaume, alisema amani haivunjiki kwa siku moja bali huanza kwa uchochezi wa maneno na vitendo miongoni mwa jamii kwa kujibizana na kupigana hali inayokwamisha maendeleo na kushuka kwa uchumi wa nchi.

Katika hatua nyingine, Dk. Mwinyi alihudhuria du'a maalumu ya kuiombea nchi kuendelea kuwa katika hali ya amani, umoja na utulivu ambayo iliandaliwa na Ofisi ya Mufti Zanzibar, iliyofanyika Masjid Rahman, Gombani Mpya, Mkoa wa Kusini Pemba.

Dua hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wananchi wa mikoa yote ya Kusini na Kaskazini, Pemba.




Dereva wa bodaboda akisafirisha abiria na mzigo wake katika eneo la King'azi, Kata ya Kwembe, Dar es Salaam jana, kitendo kinachoweza kuhatarisha usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Waziri ataja mafanikio 10 uwekezaji DP World

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imetaja mafanikio 10 yaliyopatikana kutokana na mkataba wake na Kampuni ya DP World kwa ajili ya uendeshaji wa sehemu ya Bandari ya Dar es Salaam.

Miongoni mwa mafainiko hayo ni mamlaka ya Usimamizi wa bandari Tanzania (TPA) kukusanya Sh. bilioni 325.3 kati ya Aprili na Septemba, mwaka huu.

Akiwasilisha mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 jijini Dodoma jana, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema mafanikio hayo ni pamoja na Kampuni ya DPW kuwekeza Sh. bilioni 214.425 kwa ajili ya ununuzi wa mitambo ya kisasa, ukarabati wa mitambo iliyokuwa ya TPA na usanifu na usimikaji wa mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) wa kisasa wa uendeshaji wa bandari.

Alisema DPW imenunua na kufunga vitendea kazi vya kisasa (SSG na RTG) katika kupakia na kushusha mizigo na kwamba kutokana na hatua hiyo muda wa kuhudumia meli za makasha gatini umepungua kutoka wastani wa siku saba hadi wastani wa siku tatu.

Hali hiyo, alisema imewezesha kupunguza idadi ya meli zinazosubiri angani kutoka wastani wa meli 35 Septemba, 2023 hadi wastani wa meli 15 Septemba, 2024.

Prof. Mkumbo alisema kumekuwa na ongezeko la shehena zinazohudumiwa kutoka shehena tani 141,889 mwezi Mei 2024 hadi kufikia shehena tani 168,336 mwezi Septemba 2024, ikiwa ni ongezeko la asilimia 18.6 katika kipindi cha miezi mitano.

Alitaja mafanikio mengine kuwa ni kuongezeka kwa makasha yanayohudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam gati 0 mapaka 7 kutoka wastani wa 12,000 kwa mwezi hadi 27,000 kwa Septemba, 2024.

Waziri alisema idadi hiyo ya makasha ilikuwa haijawahi kufikiwa katika historia ya Bandari ya Dar es Salaam na kwamba kiwango cha juu kabisa kabla ya hii ilikuwa ni makasha 15,000.

"Katika kipindi cha miezi mitano, gharama za matumizi ya uendeshaji wa bandari zimepungua hadi kufikia asilimia 2.7 ya makusanyo wakati matumizi yalikuwa yanaongezeka kwa asilimia 15.1 kwa mwezi kabla ya kukabidhiwa uendeshaji wa bandari kwa kampuni ya DPW," alisema

Pia alisema katika kipindi cha miezi mitano (Aprili hadi Septemba 2024) tangu DPW Dar es Salaam waanze kuendesha Gati 0-7 katika Bandari ya Dar es Salaam, serikali imeshakusanya Sh. bilioni 325.3 ikiwa ni mapato yanayotokana na shughuli za mikataba iliyoingiwa kati ya TPA na DP World, ikijumuisha tozo ya pango, tozo ya mrabaha na 'warfage'.

"Kutokana na kuongezeka kwa mapato na kupungua kwa gharama za uendeshaji kutokana na maboresho yaliyofanyika, serikali, kupitia TPA, imeanza uwekezaji katika miradi yenye thamani ya Sh. trilioni 1.922 kwa kutumia makusanyanyo yanayopatikana," alisema

Alitaja miradi hiyo ni kuwa ni ujenzi wa Kituo cha Mafuta (SRT); Ujenzi wa Bandari ya Kisiwa Mgao (Mtwara) na Ujenzi wa Gati za Majahazi Dar es Salaam.

Kuunganishwa kwa mifumo ya forodha na ile ya bandari, alisema kumewezesha kupunguzwa au kuondolewa kwa mifumo iliyokuwa inafanana, hivyo kupunguza muda wa kuondoa mizigo bandarini, kuongeza uwazi na kurahisisha mawasiliano.

Alisema mapato ya kodi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yameongezeka hadi kufikia Sh. trilioni moja kwa Septemba 2024 kulinganisha na wastani wa Sh. bilioni 850 kwa mwezi na kwamba hiyo imetokana na TRA kuchakata mizigo mingi zaidi ndani ya muda mfupi.

Alisema tangu serikali ilipoikabidhi DP World pamoja na kampuni nyingine kuendesha bandari hiyo, maboresho yanaendelea ambayo yanachochea kuongezeka kwa biashara, hivyo kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Alisema kwa kuwa mapato yameongezeka na gharama za uendeshaji kupungua serikali, kupitia TPA imeanza uwekezaji katika miradi yenye thamani ya Sh. trilioni 1.922 kwa kutumia makusanyanyo yanayopatikana.

Aliitaja miradi hiyo kuwa ni ujenzi wa Kituo cha Kupokwa Mafuta (SRT), ujenzi wa bandari ya kisiwa mgao mkoani Mtwara na ujenzi wa gati za majahazi Dar es Salaam na kuunganishwa kwa mifumo ya forodha na ya bandari.

Alisema hali hiyo imewezesha kupunguzwa kwa mifumo iliyokuwa inafanana, hivyo kupunguza muda wa kuondoa mizigo bandarini, kuongeza uwazi na kurahisisha mawasiliano.

MAENEO MATANO

Waziri huyo alitaja maeneo makuu matano ya vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2025/26 yaliyopendelezwa na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ikiwamo kuchochea uchumi shindani na shirikishi.

Alisema ili kuchochea uchumi huo pamoja na mambo mengine, serikali itaendelea na ujenzi na ukarabati miundombinu ya Reli ikiwamo SGR, kuimarishaji wa huduma za usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo, ujenzi wa miundombinu ya barabara kuu na za mikoa; barabara za kimkakati na za kupunguza foleni.

Alisema serikali itaendelea na uzalishaji wa nishati ya umeme kutoka vyanzo mbalimbali na teknolojia ya matumizi ya nishati safi usambazaji wa umeme kwa vijijini.

Pia alisema utafutaji gesi asilia na ujenzi wa miundombinu ya uchakataji wa gesi, kuimarisha utoaji wa huduma za hali ya hewa na kuendelea kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kuimarisha upatikanaji wa fedha za kigeni.

Kipaumbele kingine alisema ni kuimarisha uwezo wa uzalishaji wa bidhaa za viwandani akitaja baadhi ya vipaumbele vinavyopendekezwa kuwa ni utafutaji na uhamasishaji wa uwekezaji wa madini ya kimkakati yakiwemo madini ya chuma na magadi soda.

"Kipaumbele cha tatu ni kukuza uwekezaji na biashara ambapo serikali pamoja na mambo mengine itaimarisha mifumo kwa ajili ya kuchochea uwekezaji kwa kutunga sera, sheria,kanuni, mikakati na miongozo kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa wawekezaji katika ngazi zote," alisema.

Alitaja kipaumbele kingine ni kuchochea maendeleo ya watu, kuimarisha mifumo na usimamizi wa uendeshaji wa elimu, afya, maji na hifadhi ya mazingira ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Kingine ni kuimarisha na kuhamasisha uwekezaji katika programu za mtindo wa maisha na lishe bora, kujenga na kukarabati miundombinu ya michezo, sanaa na ubunifu

Prof. Mkumbo alitaja kipaumbele kingine kuwa ni kuendeleza rasilimali watu, kukuza ujuzi kwa vijana, kuwezesha na kuendeleza ujuzi kwa makundi mbalimbali katika ngazi zote za elimu, kuimarisha ujuzi katika majadiliano ya mikataba hususai ya mafuta, gesi na madini, uandishi wa sheria.

Pia alisema utafiti wa sheria na uendeshaji wa mashauri ya madai dhidi ya Serikali ndani na nje ya nchi; na kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Ujuzi wa Mwaka 2016/17 - 2025/26.

**•Imeandikwa na Joseph Mwendapole na Jennifer Gilla**

# Treni ya mchongoko yaanza rasmi safari za Dar hadi Dodoma

**Na Pilly Kigome**

SAFARI ya kwanza ya treni yenye kichwa mchongoko (EMU) imeanza safari zake kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma ikiwa na mabehewa manane.

Kutokana na kuanza kazi, imefanya safari za Dar es Salaam- Dodoma kuongezeka hadi nne ambapo awali zilikuwa mbili.

Akizungumza na vyombo vya habari jana Dar es Salaam katika Kituo cha Magufuli, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, alisema kutakuwa na mabadiliko ya nauli katika safari hizo.

Alisema daraja la juu nauli itakuwa Sh. 150,000 na la biashara Sh. 120,000 na kwa treni ya kawaida daraja la juu Sh. 120,000 na la biashara Sh. 70,000.

Kadogosa alisema kichwa mchongoko ni tofauti na treni za awali za kawaida kwa kuwa hutumia vichwa viwili mbele na nyuma kulinganisha na za kawaida zinazotumia kichwa kimoja na yenyewe haisimami njiani.

"Mwendo ni ule ule wa kilometa 160 kwa saa. Utofauti ni katika kuchanganya mwendo na ukimbiaji. SGR imeangalia mahitaji ya Watanzania kuanzia leo (jana) safari zitakuwa nne za kwenda na kurudi Dar es Salaam-Dodoma. TRC imejipanga sana na wanaotaka kuihujumu wajipange" alisema Kadogosa.

Aprili 3, mwaka huu, TRC ilipokea vichwa viwili vya EMU sawa na seti moja na Waziri wa Uchukuzi, Prof. Mbarawa, alisema kila kichwa kinauwezo wa kubeba mabehewa manane ambapo ni sawa na kuchukua abiria wapatao 589 kwa mabehewa yote kwa safari moja. Mbarawa alisema vichwa hivyo vimetengenezwa nchini Korea Kusini.

Meneja Mradi Ununuzi ya Treni za Mwendokasi Mtaalamu TRC, Injinia Kelvin Kimario, alisema treni hizo zitakuwa na uwezo wa kudhibiti mwendo katika hatari.

"Mfano ikipita katika maeneo ya mahandaki na maeneo hatarishi, mwendo utajidhibiti na kumwongoza dereva hata kama dereva hatapunguza mwendo, treni inauwezo kujipunguza yenyewe," alisema.

Treni hizi zitakuwa na uwezo wa kuchukua umeme mkubwa kutoka juu 25KV na hautakuwa na madhara kwa abiria.

# Serikali yaweka msisitizo utatuzi wa changamoto za vijana balehe

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imeweka msisitizo na kujidhatiti kutatua changamoto zinazowakumba vijana balehe kwa kuweka mazingira salama na rafiki kupitia afua mbalimbali zinazowawezesha kufikia malengo yao na utimilifu wao kwa ujumla.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonazi, aliyasema hayo jana Dodoma, wakati akihutubia mkutano wa wadau wanaotekeleza Afua za Vijana Balehe nchini (NAIA), kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Alisema ajenda ya kitaifa ya kuwekeza katika afya na maendeleo ya vijana balehe nchini iliyozinduliwa Aprili 17, 2021 na ilikuwa na lengo la kuharakisha utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele vinavyohusu afya na maendeleo ya vijana hao katika mikoa 13 yenye viashiria visivyoridhisha.

"Utekelezaji wa ajenda umejikita katika nguzo kuu sita, kuzuia maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU), kutokomeza mimba za utotoni, kutokomeza ukatili wa kimwili, kingono na kisaikolojia na kuboresha hali ya lishe.

"Pia kuhakikisha wavulana na wasichana wanabaki shuleni kukamilisha mzunguko wao wa elimu na kuwaendeleza vijana katika ujuzi na ufundi ili wapate fursa ya kujiari na kuajiriwa," alisema.

Alitoa rai kwa wadau wote wanaohusika na masuala ya vijana balehe kufahamu kwamba, ili kuwa na taifa imara ni vema kuwekeza katika kutatua changamoto za tabaka hilo kwa ajili ya kupata taifa imara.

"Kaulimbiu ya mkutano huu inayosema 'Ututuzi wa Changamoto za Vijana Balehe kwa Taifa Imara' inachechemua utekelezaji wa ajenda hii kwa upana wake, kwa kuwa ndiyo pekee yenye uwezo wa kukabiliana na changamoto hizo za vijana.

"Ninaamini kupitia mkutano huu, mtapata fursa ya kujadili kwa undani kuhusu changamoto zinazohusu vijana balehe kwa kutumia uzoefu wa utekelezaji wa ajenda hii kwa kipindi cha miaka mitatu," alisema Dk. Yonazi.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Wakili Amon Mpanju, alitambua juhudi za mashirika ya kimataifa na yasiyo ya kiserikali yaliyoanzisha miradi mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha vijana balehe wanapata huduma rafiki za afya, elimu,ujuzi na maarifa.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dk. Wilson Mahela, aliwakumbusha vijana kujitunza kwa kuzingatia mila na tamaduni za kitanzania zinazofaa na kuepuka kuiga kila wanachokiona katika mitandao ya kijamii.

Mwakilishi kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Edgar Lungu, aliishukuru serikali kwa kuwezesha wadau kutekeleza afua zao na kuahidi kuendelea kutoa ushirikiano, ili kufanikisha kusudio la serikali kuwa na taifa lililo na vijana imara.



Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Balozi Mhandisi Aisha Amour, akifungua Kongamano la Nne la Wanawake Makandarasi, jijini Dar es Salaam jana. Mhandisi Amour aliwahamasisha kufungua kampuni za ujenzi, ili kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Bil. 868/-kurejesha miundombinu iliyoathiriwa na El-Nino, kimbunga

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS) umetia saini mikataba 93 ya ujenzi wa barabara na madaraja yaliyoharibiwa na mvua ya El-Nino pamoja na kimbunga Hidaya.

Hivyo, kiasi cha Sh. bilioni 868.56 kinatarajiwa kutumika kujenga miundombinu ya kudumu na kurejesha mawasiliano ya uhakika.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, aliyasema hayo jana katika hafla ya utiaji saini kati ya TANROADS na makandarasi waliopata zabuni ya ujenzi wa miradi hiyo.

Alisema kiasi hicho cha fedha kinatarajiwa kutumika katika ujenzi wa madaraja na makaravati kwenye miradi hiyo 93 iliyoko mikoa yote nchini.

"Leo tumeshudia utiaji saini mikataba 93 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa madaraja na makalavati katika sehemu ambazo ziliathiriwa na mvua kwa maeneo mbalimbali nchini," alisema Bashingwa.

Alisema kutokana na mvua ya El-Nino iliyonyesha nchini kuanzia Septemba 2023 hadi Mei 2024 pamoja na kimbunga Hidaya, barabara mbalimbali za kitaifa katika mikoa 26 ziliathirika.

"Barabara 68 zilijifunga, barabara 106 zilikuwa zinapitika kwa shida na barabara 168 ziliathirika, lakini zilikuwa zinapitika kwa shida baada ya kufanyiwa matengenezo ya dharura," alisema Bashungwa.

Kadhalika, alisema maeneo hayo yaliyoathirika yalifikia kilomita 520 na madaraja na makalavani yapatayo 189 yalikuwa yamekatika na mengine kuharibika vibaya.

Waziri Bashungwa alitoa maagizo kwa TANROADS kusimamia miradi hiyo kwa karibu na kuhakikisha kuwa inakamilika kwa wakati na kwa ubora kwa mujibu wa mkataba.

"Serikali haitosita kumfukuza mkandarasi yeyote ambaye atashindwa kufikia viwango vya kazi aliyopewa," alisema Bashungwa.

Waziri huyo aliwaomba wananchi kutoa ushirikiano kwa makandarasi katika utekelezaji wa miradi hiyo na kuwa sehemu ya ulinzi wa mali za miradi na vifaa vitakavyotumika katika ujenzi.

Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Mohamed Besta, alisema kutokana na mvua iliyonyesha katika kipindi cha Septemba 2023 hadi Mei 2024, maeneo mengi yaliharibika na kusababisha barabara nyingi kutopitika.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hasssan kwa kiasi hichi cha Sh. bilioni 868.56 mkopo kutoka Benki ya Dunia, ambacho kinakwenda kujenga miundombinu ya kudumu na kurejesha mawasiliano ya uhakika," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mashabiki nendeni uwanjani kwa wingi kuishangilia Stars

**TIMU** ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), inatarajia kushuka kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam kesho ili kuwavaa wageni Sudan kuanzia saa 10:00 jioni.

Taifa Stars na Sudan zinakutana katika mechi ya marudiano ya kuwania tiketi ya kufuzu Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zitakazofanyika Februari, mwakani.

Taifa Stars, Harambee Stars ya Kenya na Uganda Cranes ya Uganda, zenyewe zimefuzu moja kwa moja kucheza fainali hizo kwa sababu ni wenyeji wa michuano hiyo.

Kanuni za Shirikisho la Soka Afrika (CAF), hutoa tiketi ya moja kwa moja kwa wenyeji, na kwa sasa imetoa tiketi kwa mataifa haya matatu kwa sababu ndio wataandaa Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027), hivyo watatumia michuano hiyo kama maandalizi ya kujiandaa na fainali za baadaye.

Katika mechi ya kwanza iliyochezwa nchini Mauritania kwa sababu wenyeji Sudan wanakabiliwa na changamoto ya hali ya usalama nyumbani kwao, ilimalizika kwa Taifa Stars kufungwa bao 1-0.

Stars inatakiwa kupambana kuhakikisha inashinda mechi hiyo na nyingine zitakazofuata kwa sababu wanahitaji kujiweka katika 'poti' nzuri kuelekea fainali hizo.

Endapo Stars itafanya vyema katika mechi ya kesho na nyingine zitakazofuata, itajiweka katika nafasi chanya ambapo haitakutana na vigogo wa Afrika, ambao wamekuwa wakipata ushindi kila wanapokutana nao.

Licha ya kikosi kilichoitwa na Kocha Mkuu, Bakari Shime, kutokuwa na wachezaji waliozoeleka, lakini bado hao waliopo wanabeba bendera ya Tanzania, hivyo mashabiki wanatakiwa kujitokeza kwa wingi kwenda kuwashangilia.

Imezoeleka kuona Stars inaundwa na wachezaji wengi kutoka Simba, Yanga au Azam, lakini safari hii imekuwa tofauti kwa sababu nyota kutoka kwa vigogo hao wameachwa ili kutosababisha kusimama kwa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Lakini pia imezingatiwa mbali na kuruhusu michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara kuendelea, lakini pia uamuzi huo utawafanya makocha wa Simba na Yanga kutopangua programu zao kwa sababu mechi za hatua ya makundi za mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho zimekaribia.

Tunaamini benchi la ufundi litafanya kazi yake vyema kwa kuwapa mbinu za ushindi wachezaji hapo kesho, lakini ili hesabu za kupata matokeo chanya katika mechi hiyo ni kwa mashabiki kutimiza wajibu wao wa kwenda kuwashangilia.

Na kwa kuonyesha umuhimu wa kipekee, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), limetangaza hakuna kiingilio chochote, hivyo shabiki jukumu lake ni kuvaa jezi ya timu hiyo na kwenda kuwashangilia kuanzia dakika ya kwanza hadi filimbi ya mwisho itakapopulizwa.

Kama mashabiki hujitokeza kujaza uwanja wakati wa matamasha ya kutambulisha wachezaji kabla ya msimu mpya haujaanza (Simba Day kwa upande wa Simba na Siku ya Mwananchi kwa Yanga), basi kesho ni siku muhimu ya kuweka historia kwa kuujaza uwanja na kuwashangilia 'askari' wetu ambao watakuwa wamebeba dhamana ya kutuwakilisha.


Pia tunawakumbusha wachezaji kufahamu thamani ya kuvaa jezi ya timu ya taifa, wakumbuke wanatakiwa kuipigania nchi bila kukata tamaa kwa kusaka matokeo chanya tu, wafahamu nafasi waliyopata si tu wataitumikia Tanzania, lakini ni nafasi nyingine kwao kujitangaza kwa kujipandisha thamani.

Mungu ibariki Taifa Stars, Mungu ibariki Tanzania kuelekea Fainali za CHAN.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com


## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Wachezaji wasipangiwe maisha, wataamua hatima yao wenyewe

**WAKATI** Ligi Kuu Tanzania Bara iko katika raundi ya 10, wapo baadhi ya wachezaji ambao wamekuwa hawapati nafasi ya kucheza katika vikosi vya timu walizopo hadi sasa.

Iwe kwa bahati nzuri, mbaya, kiwango, utovu wa nidhamu, lakini kwenye kila kikosi cha mpira wa miguu hapa duniani, wapo baadhi ya wachezaji ambao wanapati nafasi ya kutosha kutumika uwanjani.

Hapa nchini kuna timu za kati kama Dodoma Jiji, KMC, Pamba Jiji, KenGold, Fountain Gate, Tabora United, pia kuna baadhi ya wachezaji hawapati nafasi za kucheza mara kwa mara.

Hata hivyo, baadhi ya wachambuzi wa michezo wamekuwa wakiwaangalia sana wanaocheza klabu kubwa, kongwe na maarufu za Simba, Yanga na Azam.

Kama ilivyo kwa timu zingine duniani, hizo zina baadhi ya wachezaji kutokana na ushindani mkali ya namba hawapati nafasi za kucheza kwa kiasi kikubwa.

Yupo winga, Denis Nkane kwa upande wa Yanga, Kibwana Shomari na wengine, huku upande wa Simba kukiwa na kina Hussein Kazi, Ladack Chasambi, Salehe Karabaka na wengineo.

Ukiangalia wachezaji hawa siyo kama hawapati nafasi za kucheza kwenye klabu zao kwa sababu hawana uwezo, ila kuna ushindani mkubwa wa namba, hasa kuwapo kwa wachezaji kutoka nje ya nchi.

Kwa wachezaji wenye uthubutu huwa hawakimbii, bali wanavuta soksi na kupambana mazoezini kwa ajili kupigania namba. Ni kama vile tulivyoona kwa Abdulrazack Hamza ambaye wakati anasajiliwa kutoka Super Sport ya Afrika Kusini hakuna aliyedhani anaweza akapata namba mbele ya beki waa kati wa Simba, Chamou Karaboue, ambaye naye alikuwa amesajiliwa kutoka Racing Club d'Abidjan ya Ivory Coast.

Kilichotokea ni Mtanzania, Hamza ndiye amekuwa anamweka nje beki huyo kutoka nje ya Tanzania, sio kwa bahati mbaya, au upendeleo, ni uwezo tu.

Baadhi ya wachambuzi wamekuwa wakihimiza wachezaji ambao hawapati namba kuondoka kwenye timu hizo kwenda kusaka malisho katika klabu zingine.

Wamekuwa wakiwashangaa baadhi ya wachezaji ambao pamoja na kutocheza mechi yoyote, wamekuwa waking'ang'ania hapo hapo licha ya kusotea benchi.

Kwangu binafsi naona si sahihi kuwapigia kelele za kuondoka kama viongozi wa klabu na mabenchi ya ufundi bado wanawahitaji.

Kama wachezaji wanaendelea kukaa kwenye hizo timu ni kwamba wapo kama msaada kwa wale wanaocheza ili chochote kilitokea wawe tayari kusaidia. Ina maana wanahitaji na kama isingekuwa hivyo wangewaacha.

Nadhani kama mchezaji hawajaachwa na Simba, Yanga na Azam, kwangu binafsi naona hakuna haja ya kuondoka mwenyewe eti kwa sababu aende kwenye timu ambayo atakuwa anacheza tu kila siku.

Labda huyo mchezaji ajifahamu kama ana kipaji kweli kweli, lakini vinginevyo atakuwa anajimaliza.

Naelewa wachezaji wengi wanang'ang'ania Simba, Yanga au Azam kwa ajili ya maisha yao ya baadaye na si vinginevyo.

Pale wanalipwa mishahara minono na kwa wakati na posho juu, hata kama mchezo hapati namba, lakini anakusanya pesa zake kwa ajili ya maisha yake ya baadaye. Uwezo ukipungua au umri ukienda anahesabu alichokipata na kufanya mambo mengine kwa sababu angalau atakuwa amekusanya mapato.

Nafahamu, kuna wachezaji wamejuta kuondoka mapema kwenye timu hizi kwa kelele za wachambuzi wakitaka wajiunge na timu nyingine ambazo watakuwa wakionekana wiki hadi wiki. Lakini malipo yakawa hafifu pamoja na kutumika uwanjani, matokeo yake wakatoa nguvu zao bure na sasa hawana kitu.

Tuwaache wachezaji wenyewe waamue, kama wanataka kucheza tu, basi wafanye hivyo kwa hiari yao, na wale ambao wapo wanaangalia maisha zaidi hata kama hachezi anaangalia kesho yake kwani soka ni mchezo wa muda mfupi wasibezwe, yote ni maisha tu kwa jinsi wenyewe walivyoamua.

# Wasisitiza matibabu ya saratani hayaui

**Na Maulid Mmbaga**

MENEJA wa Wodi za Wagonjwa wa Uangalizi wa Karibu katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), Dk. Mwamvita Said, amewatoa hafu wananchi wanaoogopa kujitokeza kufanyiwa uchunguzi wa saratani ya matiti wakihofia kuwa matibabu ya ugonjwa huo yanaua.

Amesisitiza umuhimu wa jamii kujitokeza kwa wingi kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi kwa kuwa hiyo ndio njia pekee ya kuepukana na athari kubwa zinazotokana na maradhi hayo.

Alitoa ufafanuzi huo jana jijini Dar es Salaam wakati akipokea msaada wa vifaa vya matibabu kwa wagonjwa wa saratani vilivyotolewa na wadau wa maendeleo na afya wakiwamo Hospitali ya Shifaa, Golden Tulip na Kampuni ya Bima ya ASA.

"Si sahihi watu kusema tiba ya saratani inauwa. Muhimu ni kufanya uchunguzi na kupata matibabu sahihi. Wanaoanza kuathirika zaidi ni wanawake ambao wameanza kunyonyesha na ambao hawajaanza wanaweza kupata dalili za awali," alisema Dk. Said.

Alisema huwashauri watu wanapohisi kuwa na dalili wawahi mapema hospitalini kwa uchunguzi ili waweze kupata matibabu sahihi.

Mariam Temba kutoka Golden Tulip, alisema baada ya kukamilisha matembezi wiki iliyopita wamefanya pia, harambee na kufanikiwa kuchangisha zaidi ya Sh. milioni nane ambayo itatumika kusaidia wagonjwa wa saratani.

Victoria Tarimo kutoka Hospitali ya Shifaa, alisema hatua hiyo ni katika mwendelezo wa kuisaidia serikali katika juhudi za kutoa huduma za afya kwa jamii, huku akimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada za kuendeleza sekta ya afya.

# Watoto 85 wapatikana kwa upandikizaji mimba

**Na Mwandishi Wetu**

WATOTO 85 wamezaliwa kwa huduma ya kupandikiza mimba inayotolewa na kituo cha Kairuki Green IVF tangu kuanzishwa mwaka 2022.

Hayo yalisemwa jana Bunju Mianzini, Dar es Salaam kilipo kituo hicho na Mkurugenzi wa Kituo hicho, Dk. Clementina Kairuki, wakati mke wa Rais wa Zambia, Monica Chakwera alipotembelea kituo hicho.

Alisema huduma hiyo imeonyesha mafanikio makubwa tangu kuanzishwa kwake na kwamba mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka huu wanatarajia kufikisha watoto 100.

Ndani ya muda mfupi, alisema kutambuliwa kimataifa kwa kupata ithibati ya ubora (ISO) na kwamba wamefanikiwa kupata wateja kutoka Kongo DRC, Comoro, Marekani, Uingereza, Sweeden na mataifa mbalimbali ambao wamepata watoto na wanaendelea vizuri.

Alisema ingawa kiwango cha mafanikio ya tiba hiyo kidunia (success rate) huwa ni asilimia 45 mpaka 50, Kairuki IVF imeweza kufikisha mafanikio ya kupata watoto kwa njia ya upandikizaji na kufikia wastani wa asilimia 63.

Naye Mke wa Rais wa Malawi, Monica Chakwera, alielezea kufurahishwa kwake na huduma za upandikaji mimba inazotolewa na Kituo cha Kairuki IVF na kusema kuwa anatamani kuona huduma kama hizo zinaanza kutolewa nchini mwake.

Alisema kituo cha Kairuki IVF kimekuwa msaada kwa wanawake wengi ambao wameshindwa kupata ujauzito kwa njia ya kawaida hivyo upandikizaji umekuwa ukirudisha furaha kwa wanawake hao.

"Nimeambiwa kwamba tangu kianzishwe mwaka 2022 watoto 85 wameshapatikana kwa njia ya upandikizaji mimba. Hii ni taarifa njema sana kwani watu wengi walihangaika kupata huduma kama hizi Ulaya na mataifa yaliyondelea lakini sasa zinapatikana kwenye nchi zetu ni jambo la fahari sana.

"Sijawahi kusikia kituo kama hiki kwetu Malawi lakini ningependa kuona kinaanzishwa ili kuwapunguzia gharama watu wetu wanaolazimika kusafiri kwenda mataifa yaliyoendela kutafuta huduma kama hizi za upandikizanji mimba," alisema

Alisema anatarajia kufanya harambee kwaajili ya kupata kiasi kikubwa cha fedha zitakazotumika kuwasaidia wanawake wenye shida ya kupata watoto kutumia njia hiyo kumaliza shida zao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Kairuki, Asser Mchomvu alisema walipata wazo la kuanzisha kituo hicho baada ya kupata watu wengi wenye shida ya kupata ujauzito waliokuwa wanafika hospitali ya Kairuki Mikocheni wakitafuta huduma hiyo.

Alisema wanawake wengi wamekuwa wakiteseka kwenye ndoa zao kwa kushambuliwa na ndugu jamaa na marafiki inapotokea hajapata ujauzito wakati tatizo linaweza kuwa ni mbegu hafifu za mwanaume.

"Kwa utamaduni wa makabila mengi Afrika, mtoto asipopatikana basi wanawake wamekuwa wakionekana kuwa ndio wenye matatizo lakini kwa uhalisia wakienda kupima wanaume wengi wanakutwa na tatizo hilo. Kwa hiyo sisi tuliliona tukaona tukaona tuanzishe kituo kumaliza tatizo hilo watu wapate watoto waishi kwa furaha," alisema.




Mke wa Rais wa Malawi, Monica Chakwera (wa tatu kulia), akiwa kwenye picha ya pamoja na wageni mbalimbali, wakati alipotembelea kituo cha kupandikiza mimba cha Kairuki IVF, Bunju Mianzini, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali yaanza maandalizi awamu mpya TASAF

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema kwasasa ipo katika maandalizi ya usanifu wa awamu nyingine ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) kutokana na awamu iliyopo kufikia ukomo mwezi Septemba, 2025.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Wete (ACT-Wazalendo), Omar Ali Omar.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kufanya mapitio katika kubaini kaya maskini ili kuondoa malalamiko.

Akijibu swali hilo, Sangu alisema pia TASAF imekuwa ikitumia utaratibu wa kutambua na kuandikisha kaya maskini kupitia Mkutano Mkuu wa Kijiji, Mtaa au Shehia kwa usimamizi wa watendaji kutoka maeneo ya utekelezaji kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa na jamii husika.

Alisema katika kushughulikia malalamiko ya walengwa, wananchi na viongozi kuhusu utekelezaji wa mpango huo, TASAF imekuwa ikitumia njia mbalimbali ikiwamo kufanya uhakiki ili kuziondoa katika mpango wa kaya zilizoimarika kiuchumi.

Sangu alisema katika mapitio yaliyofanyika katika kaya 750,000 kutoka vijiji, mitaa na shehia 12,000, yalibaini kuwa kaya 394,505 zimeimarika kiuchumi na hivyo, kukidhi vigezo vya kuhitimu na kutoka katika mpango.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema katika jimbo lake kuna wananchi wametolewa kimya kimya kwenye mpango huo na kuhoji kama serikali inafahamu hilo.

Sangu akijibu swali hilo, alisema utaratibu wa TASAF ni kwamba, wale walioimarika kiuchumi kabla ya kuondolewa hupewa mafunzo na baadaye kupewa taarifa rasmi wamefikia ukomo.

"Kama jambo hili limetokea jimboni kwake ninamwelekeza mtendaji mkuu wa TASAF kulifuatilia na kama hawajataarifiwa, wataarifiwe kulingana na taratibu tulizoweka," alisema.

Kadhalika, katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti maalum (CCM), Shally Raymond, alisema maskini waliopo ni wengi wakiwamo vijana waliomaliza vyuo, wanawake na wanaume ambao hawamudu chakula katika kaya zao.

Alihoji serikali haioni ni wakati wa kutoa miradi midogo kwa makundi hayo badala ya wote kuguswa na TASAF.

Naibu Waziri Sangu akijibu swali hilo, alisema serikali imejipanga kuwezesha makundi hayo kupitia mipango mbalimbali ikiwamo Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili kuwakwamua wananchi kiuchumi.

Aidha, Mbunge wa Mwibara (CCM), Charles Kajege, alisema TASAF ni tatizo katika jimbo lake kwani, waliomo hawastahili na walio nje wanastahili.

Akijibu swali hilo, Sangu alisema utaratibu wa kuwapata wanufaika umekuwa ukifanywa kupitia mikutano ya vijiji, hivyo serikali itafuatilia suala hilo.



Mkurugenzi wa Elimu ya Juu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Peter Msofe (kulia), akiwa na Kiongozi wa Timu ya Benki ya Dunia, Prof. Roberta Malee (kushoto), wakisikiliza maelezo kutoka kwa uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Saalam (UDSM) juzi, kuhusu ujenzi wa jengo maalum litakaloshughulikia masuala yote ya Kijinsia na watu wenye ulemavu, linalojengwa kwa ufadhili wa benki hiyo, chuoni hapo.. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# UDSM kujenga jengo la kuhudumia masuala ya jinsia, wenye walemavu

**Na Grace Mwakalinga**

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimeanzisha mradi wa ujenzi wa jengo maalum litakaloshughulika na masuala ya jinsia na huduma kwa watu wenye ulemavu.

Lengo ni kutoa huduma bora kwa wanafunzi, wafanyakazi na wageni wenye mahitaji maalum.

Akizungumza wakati wa kukagua maendeleo ya mradi huo, Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma za Jinsia Chuoni hapo, Dk. Lulu Mahai, alisema jengo hilo linakusudiwa kuhudumia watu wenye ulemavu na kuwapa msaada wa kijamii na kitaaluma pamoja na kuhakikisha kila mtu anapata huduma inayostahili.

Dk. Mahai alisema jengo hilo litachangia kuwapo mazingira salama yasiyokuwa na ukatili wa kijinsia na litasaidia katika kutimiza malengo ya chuo ya kufundisha, kufanya utafiti na kujihusisha na jamii.

Kadhalika, alisema litawekewa vifaa vya kisasa vya usaidizi ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata huduma zinazokidhi mahitaji yao.

"Walemavu wa aina zote watapata eneo maalum ambalo wanaweza kufikia na kupata msaada wa kutosha kulingana na mahitaji yao maalum ikihusisha wanafunzi na wafanyakazi wenye ulemavu wa viungo, pamoja na wale wanaokabiliana na changamoto nyingine za kiafya.

"Chuo kimejitolea kuhakikisha mahali hapo panakuwa kituo salama bila kuwapo kwa unyanyasaji wa kijinsia au ukatili wa aina yoyote.

"Kituo hiki kinajumuisha dawati la jinsia ambalo litajihusisha na kushughulikia changamoto zinazohusiana na masuala ya kijinsia na kuhakikisha haki na usawa wa kijinsia kwa wanafunzi na wafanyakazi wote wa chuo kikuu," alisema Dk. Mahai.

Alisema mradi huo ni sehemu ya mipango ya muda mrefu ya UDSM iliyoko katika sera ya mwaka 2021 hadi 2061, inayolenga kuboresha masuala ya jinsia na kuhakikisha ushirikishwaji wa makundi yote katika elimu ya juu, na kwamba kitahudumia wanafunzi zaidi ya 45,000 na wafanyakazi 3,000.

Erick Nyanda, mwanafunzi mwenye ulemavu chuoni hapo, alisema kituo hicho kitatumika kama kiunganishi cha wanafunzi wenye ulemavu na wale wasio na ulemavu.

Alisema kitawawezesha wanafunzi wote kubadilishana mawazo, kushiriki michezo na kushiriki mazoezi mbalimbali ya viungo, jambo ambalo litasaidia kukuza umoja na ushirikiano miongoni mwao.

"Tutaweza kupata msaada wa moja kwa moja kwa mahitaji yetu maalum, ikiwamo ushauri wa kisaikolojia na vifaa vya kisasa vya teknolojia ya kusaidia kujifunza," alisema Erick.

Mtafsiri wa lugha za alama UDSM, Mashukura Kabwogi, alisema kituo hicho kiwasaidia wanafunzi wenye ulemavu kupata huduma stahiki na kujifunza bila vizuizi.

Alibainisha kwamba ni chuo cha kwanza kinachojenga kituo cha kutoa huduma kwa walemavu na kushughulikia masuala ya kijinsia.

Naibu Mratibu wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) kutoka UDSM, Dk. Liberato Haule, alisema chuo kimepata Dola za Kimarekani milioni 47.5, sawa na Sh. bilioni 109, kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu.

Alieleza kuwa fedha hizo zitatumika katika ujenzi wa chuo hicho katika kampasi zilizoko mikoa ya Kagera, Lindi, na Mtwara, pamoja na madarasa, mabweni, na maabara.

Dk. Haule alibainisha kuwa mitaala 98 ipo kwenye hatua za mwisho za kupata ithibati ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira, walimu 38 wamepata mafunzo ya kujifunza teknolojia mbalimbali viwandani, huku wataalam 31 kutoka sekta mbalimbali wakishiriki kutoa mafunzo kwa wanafunzi wa UDSM.

Mratibu wa Taaluma wa Taasisi ya Sayansi za Bahari na Kaimu Mkuu wa Taasisi hiyo Zanzibar, Dk. Daudi Msangameno, alisema taasisi hiyo imepokea Sh. bilioni 11 kwa ajili ya kuboresha mazingira ya ufundishaji, ikijumuisha ujenzi wa jengo la utawala na taaluma, maabara, na hosteli za wanafunzi.

Kiongozi wa Timu ya Benki ya Dunia (WB), Prof. Roberta Malee, alipongeza UDSM kujenga kituo cha kwanza cha aina hiyo kwa vyuo vikuu nchini Tanzania.

"Tuna furaha kuona maendeleo haya na dhamira mnayoweka katika kuhakikisha elimu bora kwa wanafunzi wenu wote. Hili ni jambo la kimapinduzi kwa Afrika, siyo kwa Tanzania peke yake. Tunafurahi kuona mnakuwa kigezo cha kujifunza kwa wengine duniani," alisema Prof. Malee.

Alisema mradi huo unalenga kuboresha maisha ya wanafunzi na kuwapa nafasi za kipekee za kujifunza na kukua katika mazingira yanayowajali na kuwaunga mkono.

# Wanafunzi wenye ulemavu wapata elimu maalum OUT

**Na Grace Mwakalinga**

ZAIDI ya wanafunzi 20 wenye ulemavu wa viungo, viziwi na wasioona wamepatiwa elimu maalum, inayotumia teknolojia ya kisasa kujifunza kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT).

Mpango huu unalenga kuhakikisha kuwa elimu inawafikia wote, bila kujali changamoto za ulemavu zinazowakabili, na ni sehemu ya juhudi za chuo kuboresha upatikanaji wa elimu jumuishi nchini.

Akizungumza jana kwenye ufunguzi wa mdahalo wa kitaaluma kuadhimisha miaka 30 tangu kuanzishwa kwa chuo hicho, Kaimu Makamu Mkuu wa OUT, Prof. Leonard Fweja, alieleza kuwa hatua hiyo inayendana na dhamira ya chuo hicho kutoa elimu inayokidhi mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu kwa kutumia teknolojia.

Alibainisha kuwa uwekezaji katika vifaa vya kisasa kama kompyuta na programu maalum zinazowezesha kujifunza kwa mifumo ya sauti na maandishi ni hatua muhimu katika kuwawezesha wanafunzi hawa kusoma kwa ufanisi na kushiriki kikamilifu katika masomo yao.

"Ni fahari kwetu kuona wanafunzi wenye ulemavu wakifaidika na fursa za elimu, kwani tunataka kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi, bila kujali hali yake, anapata nafasi sawa ya kujifunza na kutumia maarifa haya kwa ajili ya maendeleo ya taifa," alisema Prof. Fweja.

Aliongeza kuwa teknolojia zinazotumiwa katika mchakato wa kujifunza zinajumuisha programu zinazosaidia viziwi na wasioona kuweza kusoma na kuelewa masomo kwa urahisi zaidi. Kwa mfano, vifaa vinavyosaidia wasioona kupata taarifa kwa njia ya maandishi ya maandamano na vifaa vya kusoma vinavyojumuisha braille vinatumika, hatua inayowasaidia kupunguza changamoto walizokutana nazo awali.

Mdahalo huo ulijumuisha wadau mbalimbali kutoka sekta ya elimu na walimu wa elimu maalum ambao walisisitiza umuhimu wa kuendelea kuwekeza katika teknolojia za kisasa na programu maalum kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Wadau walipendekeza pia ushirikiano na taasisi za kimataifa ili kuongeza ujuzi na rasilimali zinazohitajika kuboresha zaidi mazingira ya kujifunza kwa wanafunzi wenye ulemavu nchini.

Katika kuhakikisha chuo hicho kinatimiza majukumu yake ya utoaji elimu nchini, Prof. Fweja alisema wanaendelea kuandaa wataalamu wa afya ya akili na ushauri nasaha ambao watasaidia taifa kukabiliana na changamoto za afya ya akili na msongo wa mawazo ambayo inagharimu maisha ya wananchi wengi.

Alisema kuwa changamoto za msongo wa mawazo na magonjwa ya akili zimekuwa zikichangia kuongezeka kwa vitendo vya kikatili katika jamii, ikiwemo mauaji, alisisitiza kuwa kuwapo kwa wataalamu wa kutosha wa saikolojia na ushauri nasaha kutasaidia kupunguza athari hizi katika jamii.

Mkuu wa Kitivo cha Elimu, Dk. Theresia Shavega, alisema katika kuadhimisha miaka 30 ya chuo hicho, wamefanikiwa kuzalisha walimu wa kutosha wanaochangia sekta elimu ndani na nje ya nchi.

Alisisitiza kuwa chuo kinaendelea na jitihada za kuboresha na kusambaza programu zake, ili kukidhi mahitaji ya soko la elimu la kisasa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa.

Naye, Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Serikali ya Wakala wa Maendeleo ya Elimu ya Uongozi Bagamoyo, Dk. Maulid Maulid, aliwahi kuwa mtumishi wa OUT Kitivo cha Elimu,alisema chuo hicho kusaidia wataalam katika sekta ya elimu kujifunza mbinu mbalimbali ili kutekeleza majukumu yao maeneo ya kazi.

Alisema hadi sasa Chuo hicho kimezalisha wataalam wengine ambao walikosa nafasi kwenye vyuo vingine kutokana na majukumu waliyokuwa nayo.

Kitivo cha elimu kimetengeneza program mbalimbali na kufanyiwa maboresho kulingana na mabadiliko ya mitaala na kisera na kutoa walimu wa ngazi mbalimbali.

"Chuo Kikuu Huria cha Tanzania si tu kinatoa wataalam wa kwenda kufundisha kuanzia ngazi ya chini hadi ya juu, pia kinatoa wataalam wanaosimamia sera na utekelezaji wa mitaala ambayo inayokwenda kutekelezwa kwenye ngazi ya kitaifa na matokeo yake yanaonekana," alisema Dk. Maulid.





# Vijana waonywa kuhusu desturi za kimagharibi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

VIJANA wameaswa kuacha kuiga kila wanachokiona kwenye mitandao ya kijamii huku wakishauriwa kujitunza kwa kuzingatia mila na desturi za kitanzania zinazofaa.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Wilson Mahela, alisema hayo juzi kwenye mkutano wa wadau wanaotekeleza afua za vijana balehe nchini (NAIA).

Dk. Mahela alisema vijana hawapaswi kuendelea kuiga kila kitu wanacho kiona kwenye mitandao ya kijamii bali waendelee kuishi kwenye misingi ya mila na tamaduni za kitanzania.

Alisema hivi sasa kumekuwa na wimbi kubwa la vijana kuiga mambo ambayo si mila na utamaduni wa Kitanzania hali ambayo inachangia ongzeko la mmonyoko wa maadili.

Akifungua mkutano huo, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera ,Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonazi, alitoa rai kwa wadau wote wanaohusika na masuala ya vijana balehe kufahamu kwamba ili kuwa na taifa imara ni vyema kuwekeza katika kutatua changamoto za kundi hilo.

Pia alisema serikali imejidhatiti kutatua changamoto zinazowakumba vijana balehe kwa kuweka mazingira salama na rafiki kupitia afua mbalimbali ili kufikia malengo.

"Kaulimbiu ya mkutano huu inasema 'Utatuzi wa Changamoto za Vijana Balehe kwa Taifa Imara' inachechemua utekelezaji wa ajenda hii kwa upana wake kwa kuwa ndiyo pekee yenye uwezo wa kukabiliana na changamoto hizo za vijana kwa sasa.

"Hivyo ni matumaini yangu kuwa kupitia mkutano huu, mtapata fursa ya kujadili kwa undani kuhusu changamoto zinazohusu vijana balehe kwa kutumia uzoefu wa utekelezaji wa Ajenda hii kwa kipindi cha miaka mitatu," alisema Dk. Yonazi.

Pia alisema utekelezaji wa ajenda hiyo umejikita katika nguzo kuu sita ikiwemo kuzuia maambukizi ya VVU, kutokomeza mimba za utotoni, kutokomeza ukatili wa kimwili, kingono na kisaikolojia, kuboresha hali ya lishe, kuhakikisha wavulana na wasichana wanabaki shuleni.

Naye Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Wakili Amon Mpanju, alisema serikali inatambua juhudi za mashirika ya kimataifa na mashirika yasiyo ya kiserikali yaliyoanzisha miradi mbalimbali kuhakikisha vijana balehe wanapata huduma rafiki za afya, elimu ya afya ya uzazi na kupata ujuzi na maarifa ya kuwafanya wamudu maisha yao.

# Aweso ataka utafiti vyanzo vipya maji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KUTOKANA na ongezeko la mgawo mkali wa maji uliopo hivi sasa katika jiji la Dodoma, Waziri wa Maji, Juma Aweso, amewaagiza wataalam wa wizara hiyo kufanya utafiti wa kina ili kuwezesha kuchimbwa kwa visima vya maji ambavyo vitasaidia kupunguza hali hiyo.

Aweso alitoa maagizo hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na wakazi wa kata ya Nkuhungu alipofanya ziara ya kukagua maeneo yenye upungufu mkubwa wa maji.

Alisema pamoja na uwapo wa mipango ya muda mrefu ya serikali ikiwamo kuleta maji kutoka Ziwa Victoria na ujenzi wa bwawa la Farkwa, wananchi hawawezi kuendelea kusubiri bali inapaswa kutafutwa njia mbadala ya kutatua kero hiyo.

"Maji hayana mbadala hatuwezi kusubiri hadi miradi hiyo mikubwa ikamilike bali tunapaswa kuhakikisha kuwa utafiti unafanyika ili kuchimbwa visima ambavyo vitasaidia upatikanaji wa uhakika wa maji kwa wananchi," alisema Aweso.

Pia alisema utafiti huo unapaswa kuanza haraka iwezekanavyo ili visima vichimbwe na watu kuanza kupata maji ili kuondokana na adha iliyopo sasa.

"Furaha yangu nikiwa waziri ni kuona watu wanapata maji na si vinginevyo na hakuna jibu la kumpa mtu ambaye hapati maji zaidi ya kumpatia maji hivyo basi mimi sitakuwa kikwazo cha wananchi kukosa maji," alisema Aweso.

> **"Mheshimiwa Waziri wa Maji nashukuru sana kwa kukubali kuja kufanya ziara katika jiji la Dodoma kukagua maeneo yenye changamoto kubwa ya maji jiji hili linakua kwa kasi...**

Waziri Aweso pia alisema mamlaka za maji nchini zinapaswa kuanza matumizi ya mita za malipo kabla ili kuondoa malalamiko ya wananchi kubambikiziwa ankara za maji.

"Mita za Luku kwenye mamlaka za maji nchini ndiyo suluhu ya watu kumbambikiziwa bili kumekuwepo na malalamiko mengi unakuta mtu hapati maji miezi mitatu lakini bili inakuja Sh. 100,000. Hii si sahihi lazima tubadilike kwenye matumizi ya teknolojia," alisema.

Waziri wa Madini na Mbunge wa Dodoma Mjini, Antony Mavunde, aliishuru serikali kwa jitihada ambazo inafanya kutatua tatizo la maji katika jiji la Dodoma.

"Mheshimiwa Waziri wa Maji nashukuru sana kwa kukubali kuja kufanya ziara katika jiji la Dodoma kukagua maeneo yenye changamoto kubwa ya maji jiji hili linakua kwa kasi sana hivyo mahitaji ya maji yameongezeka maradufu.

"Lakini namshkuru Rais Samia Suluhu Hassan akiwa katika ziara yake mikoa ya nyanda za juu kusini alipopita hapa Dodoma tulimuomba visima ili kupunguza kero hii ya mgao iliyopo akatukubalia hivyo kupitia wataalam wako tunaomba tupate visima ili kupunguza changamoto hii", alisema Mavunde

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), Mhandisi Aron Joseph, alisema mahitaji ya maji katika jiji la Dodoma ni lita milioni 147 kwa siku huku uzalishaji ukiwa ni lita milioni 79, hivyo kufanya upungufu kuwa lita milioni 68 kwa siku.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo akiwasilisha mapendekezo ya mpango wa maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/2026, bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TFRA yahamasisha matumizi sahihi ya mbolea

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KUELEKEA msimu wa kilimo 2024/25 Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imejipanga kuendelea kuhamasisha wakulima kutumia pembejeo ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, alisema jana wakati akielezea fursa za upatikanaji wa mbolea ya ruzuku inayotolewa na serikali kwa wakulima kwa ajili ya matumizi ya kilimo.

Laurent alisema Tanzania ina fursa za uwekezaji wa viwanda vya mbolea, hivyo wakulima watumie nafasi hiyo ya upatikanaji wa mbolea ya ruzuku ili kuondokana na kilimo cha kujikimu badala yake wafanye kilimo chenye tija cha kujiinua kiuchumi.

Alisema ardhi iliyopo ni lazima wakulima watumie mbolea ili kuzalisha mazao mengi kwa ajili ya mahitaji ya chakula na biashara lakini pia wataongeza uzalishaji ambao utawasaidia kujiinua kiuchumi. Alisema ni muhimu wakulima kujenga utaratibu wa kutumia mbolea ili kuondokana na kilimo cha kujikimu na kujikita kwenye kilimo cha matumizi sahihi ya mbolea ambacho kitaleta mapinduzi kwenye sekta hiyo.

"Kilimo kinaboreshwa na matumizi sahihi ya mbolea. Karne ya sasa mbolea ni muhimu ili kufanya kilimo chenye tija na ushindani katika uzalishaji," alisema Laurent.

Alisema wakulima wakifanya hivyo kwa kutumia mazingira wezeshi yaliyopo kwenye kilimo watazidi kuchochea dira ya mwelekeo wa uchumi wa nchi ili kufikia malengo ya kujitosheleza kwa chakula. Aliaema TFRA itaendelea na kampeni ya utoaji elimu kwa wakulima ya umuhimu wa matumizi sahihi ya mbolea katika kilimo ambacho wakulima wanafanya.

Matumizi ya mbolea, alisema ni muhimu kutokana na sababu za ongezeko la watu ambalo linahitaji uzalishaji wa chakula kingi ili kusaidia kukidhi mahitaji kwenye maeneo mbalimbali.

Mkurugenzi huyo alisema serikali tayari imechukua hatua za kuimarisha matumizi sahihi ya mbolea,hivyo wakulima nao wanapaswa kutumia fursa hizo ili kujiinua kiuchumi kupitia kilimo.

Naye mtaalam mbobezi wa taaluma ya udongo kutoka TFRA, Dk. Ashery Kalala, alisema kwa kawaida inahitajika kuweka mbolea kwenye mmea kulingana na mahitaji.

Alisema wakulima wanapaswa kupewa elimu pia kuhusu aina za udongo wanaotumia ili waweze kujua ni aina gani ya mbolea wanapaswa kutumia ili kuzalisha kwa wingi.





# BLW yasisitiza upandaji mikoko

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMATI ya Baraza la Wawakilishi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, imeitaka Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na taasisi zinazoshughulikia mazingira kudhibiti athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kuotesha miti aina ya mikoko ili kuzuia kasi ya maji ya bahari kuingia nchi kavu na kutishia maisha ya wananchi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Machano Othman Said, alisema jana alipokutana na uongozi wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inayoshughulikia mazingira na taasisi zake katika kufuatilia athari za mazingira kukabiliana na tishio la mabadiliko ya tabianchi.

Machano alisema kisiwa cha Pemba kimeathirika na mabadiliko ya tabianchi na juhudi za makusudi zinahitajika ili kuzuia janga hilo na kuepuka kusababisha maafa makubwa.

Alisema maeneo ambayo wananchi walikuwa wakifanya shughuli za kilimo, hivi sasa yameingiliwa na maji ya chumvi na kuwafanya kusitisha kazi zao ambazo ndizo tegemeo katika kupata kipato na uchumi.

Aliitaka ofisi hiyo na mamlaka zinazoshughulikia mazingira na asasi za kiraia kuongeza juhudi za kupanda mikoko ili kuzuia athari zaidi za maji ya bahari kuja juu na kutishia wananchi kuyakimbia makazi yao.

"Wajumbe wa kamati ya viongozi wakuu wa kitaifa kazi yetu kubwa ni kufuatilia na kuangalia athari zinazokikabili kisiwa cha Pemba zinazotokana na mabadiliko yatabia ya nchi na uharibifu wa mazingira"alisema.

Ofisa Mdhamini Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais Pemba, Ahmed Othman, aliyataja maeneo ya Sipwese kuwa yameingiliwa na maji ya chumvi, hivyo wananchi kuacha shughuli za kilimo.

Alisema juhudi za makusudi zimechukuliwa ikiwamo kujenga tuta ambalo litazuia maji ya chumvi kuingia katika mashamba ya wakulima.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, alisema kuna takribani maeneo 148 Unguja na Pemba yanakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuwafanya baadhi ya wakazi wake kuyakimbiya.

Alikitaja Kisiwa Panza kilikocho Pemba na Mtambwe Mkuu kuwa vimeathirika na mabadiliko ya tabianchi ambayo kwa kiasi kikubwa yamesababishwa na wananchi kufanya uharibifu mkubwa wa mazingira ikiwamo kukata mikoko.

# Hemed asisitiza kazi ya SMZ ni kuwatumikia wananchi wote

**Na Mwandishi Wetu,**
PEMBA

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Hemed Suleiman Abdulla, amesema kazi ya serikali ni kuwatumikia Wazanzibari hasa katika kuwaletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Hemed aliyasema hayo kwenye ufunguzi wa kongamano la kumpongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, lililoandaliwa na Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) lililofanyika katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Wete kisiwani Pemba.

Alisema ni wajibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kuwatumikia wananchi wa Zanzibar ili wafikie malengo yao ya kiuchumi na kijamii bila ubaguzi wowote.

Hemed alisema serikali itaendela kuwafikia na kuwawezesha wajasiriamali wote ili kufanya kazi zao katika mazingira mazuri na kukuza mitaji ya biashara kwa faida zao na taifa kwa ujumla.

Hemed ambaye pia ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, alisema miradi mbalimbali inayoendelea na ujenzi na iliyokwishajengwa ni uthibitisho kwamba serikali ina nia ya dhati kuwapelekea wananchi maendeleo ikizingatiwa kuwa kila mwananchi wa Unguja na Pemba atafaidika na miradi hiyo.

Pia aliwataka UWT kufanya kazi ya kuitafutia kura za ushindi CCM kwa kuwashajihisha wananchi kujiandikisha katika daftari la kupiga kura ili kupata fursa ya kuipigia kura CCM na kuendelea kushikilia dola ifikapo mwaka 2025.

Naye Makamu Mwenyekiti wa UWT Taifa, Zainab Khamis Shomari, alisema utekelezaji wa ilani katika kipengele cha kuwawezesha wanawake kimetekelezwa kwa kiasi kikubwa na wanawake wamekuwa wakinufaika kupitia programu mbalimbali zinazotekelezwa na serikali za kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Shomari alisema UWT imejipanga kuwafikia na kuwawezesha wanawake wengi wa Zanzibar kwa kuwapatia mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 75 zitakazotolewa katika mkoa wa Kaskazini Pemba na Sh. milioni 170 kwa Pemba nzima.

Katibu Mkuu wa UWT, Suzan Peter Kunambi, alisema serikali imefanya mambo mengi ambayo yanawanufaisha wanawake katika nyanja mbali mbali za kiuchumi na kijamii ndani ya Zanzibar. kunambi alisema wanawake wa UWT watahakikisha Dk. Mwinyi anapata kura nyingi za heshima zitakazomwezesha kuendelea kuiongoza Zanzibar na kuwaletea maendeleo wananchi wake kwa miaka mitamo mingine.

Aliiomba serikali kuendelea kuwatumia wataalam wanawake katika harakati mbalimbali za chama na serikali ikiwamo kuwapa nafasi na kuwaamini katika kusimamia miradi ya maendeleo inayoendelea kujengwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla ikiwa ni kuunga mkono jitihada za serikali za kuwawezesha wanawake kiuchumi.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Juma Pembe (kushoto), akizungumza wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Kwanza wa Jukwaa la Wanawake katika usafiri wa anga Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi 3,577 walipwa fidia uchimbaji mafuta

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Shaaban Ali Othman, amesema wananchi 3,577 wamelipwa fidia kutokana na nyumba zao kuathirika na mitetemeko ya uchimbaji mafuta na gesi asilia.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana katika ukumbi wa Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) kuhusu mafanikio ya wizara hiyo kuelekea miaka minne ya uongozi wa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema idadi hiyo ya wananchi waliolipwa fidia ni sawa na asilimia 83. Waziri Shaaban alisema Mamlaka ya Udhibiti na Ufuatiliaji Mafuta na Gesi Asilia inaendelea na hatua za kuwalipa wananchi waliokuwa hawajalipwa kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Pia alisema Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, imepata mafanikio mbalimbali ikiwamo soko la kisasa katika eneo la Malindi ambalo kwa sasa linahudumia zaidi ya watu 10,000.


Pia alisema wizara hiyo imefanikisha kujenga kiwanda cha kusarifu mwani katika eneo la Chamanangwe, Pemba chenye uwezo wa kuchakata mwani mkavu kwa mwaka.

Alisema katika kipindi cha miaka minne, wizara imejenga wa kiwanda cha kutengeneza chakula cha samaki katika eneo la Kama chenye uwezo wa kuzalisha tani tano kwa siku.

Waziri Shaaban alisema miongoni mwa mafanikio ya miaka minne ni pamoja na marekebisho ya Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia ili kuvutia wawekezaji Zanzibar.

Pia alisema wizara imegawa boti 1,927 kwa Unguja na Pemba na kati ya hizo, asilimia 70 za vijana na asilimia 90 za ukulima wa mwani ambazo wanufaika ni mwanawake.

Alisema mapato yatokanayo na tozo katika sekta ya uvuvi na uhifadhi yameengezeka kwa kutoka Sh. bilioni 1.65 mwaka 2021 hadi Sh. bilioni 6.0 kwa mwaka 2023.



ZUCHU
UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI NOVEMBA 2, 2024



# HAKUNA UJANJA TENA
# Ushahidi mpya Diddy hatoki

KATIKA hali ya kushtua zaidi, shahidi mpya katika kesi inayomkabili rapa maarufu wa Marekani, Sean "Diddy" Combs, amejitokeza akiwa na ushahidi unaowahusisha watu mashuhuri waliofanyiwa vitendo vichafu na msanii huyo.

Shahidi huyo ambaye jina lake limefichwa, ametoa ushahidi huo mbele ya mahakama kuu ya shirikisho ya Manhattan.

Hata hivyo, Diddy alikuwa katika kizuizi cha Metropolitan huko Brooklyn, akisubiri muda wa kusikilizwa Mei 5, 2025.

Wakili anayewatetea waathirika, Ariel Mitchell alishiriki na waandishi wa habari kuwa mteja wake huyo mpya ana ushahidi muhimu ikiwamo video hiyo inayowashirikisha watu mashuhuri ambao huenda nao walidhulumiwa.

Kulingana na kituo cha CNN, Mitchell alithibitisha kwamba Idara ya Usalama iliwasiliana kwanza na shahidi huyo wakati wa uchunguzi.

"Mteja wangu aliitwa na ana ushahidi unaohitajika kuthibitisha kwamba madai yake dhidi ya Diddy ni ya kweli." Alisema.

Shahidi huyo pia alisema ana maandishi ambayo yahaririwa kutoka kwa Kim Porter, mpenzi wa zamani wa Diddy na mama wa watoto wake wanne.

BASI SAWA

## Mrembo Rwanda hachomoki



PAMOJA na kushinda taji la Miss Rwanda, Divine Muheto, hajanusurika kukabiliana na mkono wa sheria, kwani kwa sasa anakabiliwa na adhabu ya kifungo au kulipa faini kwa kosa la kuendesha gari akiwa amelewa.

Mrembo huyo ambaye ni maarufu tangu apate taji hilo 2022, inaelezwa hawezi kunasuka katika mashtaka hayo baada ya vithibitisho kuonyesha kuwa alikutwa anaendesha gari akiwa amelewa tena bila leseni na kusababisha ajali.

## Mrembo amzawadia iPhone Otile Brown



MWANAMUZIKI wa Kenya, Otile Brown, amekuwa na furaha baada ya kutumiwa zawadi ya simu aina ya iPhone 16 na mrembo kutoka Marekani.

Brown ambaye mara kadhaa anaonyesha zawadi anazopewa na mashabiki zake kupitia mitandao ya kijamii, amesema kutokana na ladha nzuri ya muziki wake anajivunia kupata wafuasi wenye upendo na kujitoa kwake.

Asante sana Malkia kwa zawadi ya iPhone. Umefanya kwa siku yangu muhimu, Mungu akubariki," ameandika Brown.




# SIRI ZAMWAGWA BIFU LA ZUCHU, WAKAZI

BIFU kali linaloendelea kati ya wasanii wawili wa Bongo Fleva, Zuchu na Wakazi, limeibua siri mpya baada ya wanamuziki hao kuanza kutoleana siri zao.

Zuchu na Wakazi wamekuwa katika vita vya maneno baada ya kuwepo kwa mjadala uliolibuliwa katika mtandao wa X, pale mfuasi mmoja alipotoa maoni yake kwamba Zuchu anaweza kutunga nyimbo kuliko Lady Jaydee.

Baada ya mjadala mkali kuhusu ulinganisho huo, ndipo Wakazi alipomtetea Jaydee na kumtaka Zuchu kukemea suala hilo hadharani, kitendo ambacho kilimkera Zuchu na kuanza kupeana maneno makali.

Kama haitoshi, Wakazi jana alitoa siri kwamba Zuchu ambaye anakana kuzijua nyimbo zake, alimuomba amsindikize Zanzibar na kumlipia kila kitu ikiwamo tiketi ya ndege na hoteli ya gharama kubwa.



# 'Trace Music Awards' kuleta mapinduzi Bongo Fleva

WASANII maarufu barani Afrika watakusanyika katika visiwa vya Zanzibar, kushuhudia sherehe za utoaji tuzo za Trace Music zitakazofanyika kwa siku mbili.

Tamasha hilo ambalo litafanyika Februari 24 hadi 26 mwakani litashuhudia kuwepo kwa kipengele kipya cha Muziki wa Bongofleva ili kutoa nafasi kwa wasanii wa Tanzania kujitangaza kimataifa.

Utoaji wa tuzo hizo zitashuhudiwa na nchi zaidi ya 120 kupitia channel ya Trace ambayo ndio waandaji wa Tuzo hizo.

# MSIFIE MKEO BABU WE

**Na Adam Fungamwango**

MARA nyingi duniani mtu hukisifu kilicho chake na ni vizuri kukisifu unachokipenda. Sijajua kama wasanii wa muziki wa kizazi kipya kwenye nyimbo zao ambazo asilimia 90 na zaidi zimelenga kwenye mapenzi kama kuna yeyote ambaye amemtungia mpenzi wake wa kweli au mkewe, huku akimtaja jina kwenye wimbo.

Sitaki kuingia kwa undani sana kujua ambao huwa wanawaimba ni akina nani, lakini wanamuziki na dansi wa zamani pamoja na asilimia kubwa kutunga nyimbo zenye matukio ya kweli, lakini pia walikuwa wanatunga nyimbo za kuwasifu wapenzi au wake zao.

Na wala halikuwa hawafichi, hivyo hata mashabiki wao walikuwa wanajua kabisa kuwa wimbo huu mtunzi au mwimbaji fulani amemuimba mkewe.

### Asha Mwanasefu-TX Moshi William

Ndiye mwanamuziki anayeongoza kwa kumtungia mkewe nyimbo nyingi kuliko mwingine yeyote. Alimtungia nyimbo tatu.

Tx Moshi William aliyefariki mwaka 200[illegible] akiwa na bendi ya Msondo Ngoma Music, wakati anaingia tu kwenye bendi hiyo mwaka 1982, ikiitwa Juwata Jazz, alimtungia mkewe Asha Sefu wimbo unaitwa 'Hamida'. Hilo pia ni jina la mkewe huyo huyo. Baadaye akatunga wimbo unaitwa 'Asha Mwanasefu', jina amabalo ni maarufu zaidi na hata wimbo huo ukawa maarufu zaidi kuliko nyingine alizomtungia.

Wimbo mwingine aliyemtungia mkewe huyo huyo wimbo unaitwa 'Cheusi Magala' Magala ni jina pia la kiasili la mkewe huyo huyo, Asha.

### Lucy Bandawe-Athumani Momba

Huyu ni mwanamuizik aliyepitia bendi nyingi kama vile Dar International, Vijana Jazz, Bima Lee na Msondo Ngoma Music.

Akiwa na Msondo alimtungia mkewe wimbo uliioitwao 'Lucy Bandawe'. 'Lucy Bandawe nipeleke Nyasa..." ni moja kati mashairi yaliyomo kwenye wimbo huo aliyomtungia mkewe. Lucy ni mwanamichezo wa zamani, kwani alikuwa mashuhuri kwenye mchezo wa netiboli alizichezea klabu mbalimbali za zamani.

"Alipokuwa anatunga alinificha, nikiingia chumbani wakati anaandika au kuimba ananifukuza, sikujua ni nini, baadaye nikagundua kumbe ndiyo alikuwa anautayarisha wimbo huu. Hakutaka nijue, alitaka kunifanyia 'sapraizi'." Anasema Lucy.

Momba mwimbaji wa sauti kali ya kwanza kiasi cha kubatizwa jina 'sauti ya chuma', alifariki dunia 2005

### Zarina-Hassan Bitchuka

Ni wimbo wa 'Zarina' ulipigwa katikati ya miaka ya 1970. Ni kipindi ambacho bendi hiyo inatoka kuitwa Nuta jazz na kuwa Juwata Jazz wana Msondo Ngoma.

Kwa mujibu wake mwenyewe anasema alimtungia na kumuimbia mkewe, hivyo naye anaingia kwenye kundi la wanamuziki waliowatungia nyimbo wake zao.

### Mama Feri-Cosmas Chidumule

Mwanamuziki huyu wa zamani wa bendi za Butiama, Western, Kurugenzi, akiwa na bendi ya DDC Mlimani Park aliwa hukutunga wimbo unaitwa 'Mama Feri'. Huu alimtungia mkewe Cecilia Michael wakati huo miaka ya 1980.

"Kumbe hata kwa ndugu zako umefikisha malalamiko yako, eti nina mpango wa kuoa mke mwingine, badala yako, wazo hilo sina mama..." Yalikuwa ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo.

Chudumule kwa sasa ameachana na nyimbo za kidunia na kujikita kwenye nyimbo za Injili.

### Tulele Tuboe-Mikidadi Seif

Alikuwa ni mwanamuziki wa bendi ya Uda Jazz ambaye alifariki hivi karibuni mkoani Ligi. Mikidadi kwenye miaka ya 1980 alitunga wimbo wa 'Tulele Tuboe'. Alimtungia aliyekuwa mkewe Suzana Makota kuwa waishi walee watoto.

Wimbo huo aliutunga na kuuimba kwa lugha ya Kimwera.

FILAMU

# Amaria: Ua kwa upanga, ufe na upanga

**Na Adam Fungamwango**

'AMARIA', ni filamu inayoonesha jinsi jamii zetu zinavyoweza kuingia kwenye mzozo au ugomvi na jamii, familia au jirani.

Ugomvi huo unaweza kutokana na vitu vilivyo dhahiri au vilivyojificha vinafanyika bila wenyewe kufahamu.

Wapo watu wanaoingizwa kwenye mgogoro bila wao kujijua.

Imechezwa na baadhi ya wasanii ambao ni Shukurani John, Hans Popa, Abdul Khalfan, Kassim Mbwembwe, Elizabeth Kombe, Mrs Ngokwe, Sweet Balih, Lucy Habaru, Jasmine Waziri na wengineo.

Inaanza kwa kuonesha kuwa kijana Nyayo ana uhusiano wa kimapenzi na msichana Amaria kwenye kijiji fulani hivi.

Inavyoonekana ni kama wazazi wa pande zote mbili walikuwa hawapendi uhusiano wa watoto wao. Ikawa ni kupigana mikwara tu. Kila mzazi wa mmoja anapokutana na mkwewe anampiga mkwara kuwa na uhusiano na mwanaye.

Amaria anapata ujauzito. Anapoupata tu, Nyayo anabadilika. Hamtaki tena Amaria. Amaria anaumia na kuteseka, kwani ana kiumbe tumboni, lakini pia mpenzi wake amemkataa.

Mama Amaria, Bi. Ndoza anakasirika sana juu ya binti yake kupewa ujauzito na kutelekezwa. Anaahidi kulipa kisasi.

Nyayo anatangaza ndoa na mwanamke mwingine. Siku ya ndoa ndiyo inakuwa siku ya maafa, kwani mama yake anakufa kwa kurogwa na mama Amaria.

Halafu bwana harusi naye anakufa kutokana na husuda ya mama Amaria anayelipiza kisasi.

Kijiji sasa kinaanza kutafuta mtu anayefanya matukio hayo. Anakuja mama mmoja ambaye anakuja kumaliza utata.

Mama huyo ndiye mkuu wa uchawi kwenye kijiji jirani. Anafichua siri kuwa mama Amaria alifika kwake zamani kusaka uchawi, akapewa masharti uzao wake kwa kwanza aupeleke huko, lakini hakutekeleza, kwani baada ya kumzaa Amaria hakufanya hivyo.

Na kama haitoshi uchawi huo akautumia kwa manufaa yake, hivyo anafaa kuadhibiwa na Amaria akijifungua akijifungua mtoto atachukuliwa kufidia masharti yaliyowekwa.

Habari nzuri ni kwamba Nyayo na mama yake kumbe hawakufa, ila walichuliwa kiuchawi, hivyo wakarudishwa, Bi. Ndoza aliadhibiwa hapo hapo kwa kuchomwa moto akiwa hai.




# Tems ajutia umaarufu

MSANII wa Nigeria, Tems amefunguka kuhusu jinsi umaarufu ulivyombadilisha kwa kiasi kikubwa utaratibu wake wa maisha ya kila siku.

Amesema sehemu fulani ameathirika hasa kuwa na uhuru wa kutembea katika mitaa ya jiji la Logos, ambao kwa sasa hawezi tena.

"Mimi ni maarufu sana nyumbani, kwa hivyo siwezi kwenda popote. Wanajua mimi ni nani, kwa hivyo siwezi kuendesha popote. Nilikuwa nikijaribu kuendesha gari hapo awali lakini karibu nipatwe na matatizo  mwaka jana kwa sababu nilikuwa mwenyewe," amesema Tems.





## Tiwa Savage atetea jina lake

MWANAMUZIKI kutoka Nigeria, Tiwa Savage, ameamua kujitokeza na kueleza kwamba sio sahihi yeye ana matendo ya ajabu.

Katika mahojiano yake ya hivi karibuni, mwimbaji huyo alifafanua kuwa, licha ya jina lake la kisanii kueleweka vibaya, lakini hana tabia mbaya kama wanavyofikiri wengi.

"Hakika mimi ni msichana mwenye mpenzi,

mara nyingi watu wanapokutana nami ana kwa ana wanadhani mimi nina tabia mbaya kwa sababu ya jina langu, lakini ni kinyume kabisa," amesema.

## Skales awavimbia polisi

MSANII wa Nigeria, Skales ameelezea kusikitishwa kwake na polisi wa nchi hiyo kutokana na kuweka vituo vingi vya ukaguzi barabarani.

Akitumia ukurasa wake wa X, Skales amelalamikia hatua hiyo kuwa ni matumizi mabaya ya mamlaka.

"Chuki yangu kwa polisi wa Nigeria bado ni watu wa kutisha sana, polisi wasio na pesa wanawaumiza masikini wenzao kwa kuwaomba rushwa," ameandika Skales.





## Ndoto yake Rihanna kupata mtoto wa kike

MWANAMUZIKI maarufu kutoka Marekani, Rihanna amesema itakuwa jambo la furaha zaidi kama mtoto wa tatu atakuwa msichana.

Rihanna na mpenzi wake, ASAP Rocky, wana watoto wawili wa kiume Riot na RZA, ambao wanawalea kwa mapenzi makubwa.


"Nataka kuwa na msichana, lakini siwezi kujua nini la kufanya kwa sababu kwa sasa ninajua kuhusu watoto wa kiume, lakini kama nitafanikiwa itakuwa jambo la kusisimua," amesema.

## Ayra atamani kuchumbiwa

STAA wa muziki wa Afrobeats, Ayra Starr, ambaye hajawahi kuishi maisha ya uchumba, amesema akimpata mtu wa aina hiyo atajivunia kuwa katika tasnia ya muziki.

Akizungumza na mwimbaji wa Marekani Coco Jones, Ayra amesema atakuwa kama yuko kwenye ndoto kuishi katika maisha ya uchumba ambayo kila kitu lazima kushirikiana.

Amesema anawaona watu walio kwenye uhusiano wanaishi kwa furaha, hivyo anatamani siku moja kuwa na maisha kama hayo.





# Wadaiwa kutelekeza familia kisa ulevi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

ASILIMIA 30 ya wanaume, wakazi wa vijiji vya Kuruweni na Mawanda, kata ya Mwika Kusini, wilaya ya Moshi, wanadaiwa kutelekeza familia zao kutokana na ulevi uliokithiri. Pia imeelezwa kuwa baadhi yao wanatuhumiwa kulazimisha kupewa na wengine kuchukua kwa nguvu mavuno ya fedha zinazotokana na michango ya wake zao kwenye vikundi vya vikoba.

Vilevile, inaelezwa kuwa baadhi ya wanaume wa eneo hilo, wanaathiriwa na masuala ya ushirikina kutokana na wanawake kuzidiana kiuchumi na kupora waume wa wenzao katika mazingira ya ushirikina.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Kiuchumi cha Upendo, Danson Mariki, akizungumza jana katika kikao kazi cha wadau wa Mradi wa Sauti ya Haki, alisema ulevi huo umekuwa chanzo kikuu cha kuongezeka matukio ya ubakaji dhidi ya wanawake na ulawiti dhidi ya watoto.

Mradi huo unatekelezwa na Shirika la kiraia la KWIECO, linalofadhiliwa na Women Fund Tanzania Trust (WFT), "Tumefikia hatua ambayo jamii inaumia, wengine wana kufa vifo vya ajabu kwa sababu ya ulevi. Vijana wanashindwa kufanya kazi za kujitolea kwa sababu ya kukosa nguvu, yote ni sababu ya ulevi," alisema Mariki.

Aidha, Elvenet Mlaki, alisema matukio mengi ya ubakaji, ulawiti wa watoto na umasikini, yanasababishwa na imani potofu na vitendo vya ulevi wa kupindukia.

Kutokana na hali hiyo, Esther Temba alisema baadhi ya mambo yanayowekewa mkazo, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu na kukemea ulevi kupindukia, ubakaji, ulawiti, unyanyasaji wa kijinsia, matumizi ya dawa za kulevya na wanafunzi kukatisha masomo.

Temba alisema baadhi ya vijana pia katika eneo hilo, hasa wasichana wanatajwa kutotaka kuolewa, wakiamini kuwa kuzaa na kulea mwenyewe (single mother), ni bora zaidi ya kuishi na mume.

Ofisa Ufuatiliaji, Tathimini na Taarifa wa KWIECO, Peter Mashingia, akitoaelimukwa kikundi hicho, alisema mume kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1970, analo jukumu la msingi la kutunza familia; huku akieleza sababu hiyo imekuwa kichocheo cha kukua kwa ukatili wa kiuchumi.

Pia aliwataka wanawake na vijana waliochukua fomu za kugombea uchaguzi wa serikali za mitaa, kutambua wajibu wao kwa sababu mwakilishi wa wananchi ambaye ni kiongozi wa kisiasa, anabeba hatma ya watu wake kwa miaka yote atakayokuwa madarakani.

"Unapotaka kugombea hizi nafasi, hebu waza utatengenezaje mifumo ya kuhakikisha kwamba kuna upatikanaji wa fursa mtawalia, ili vijana na wanawake waweze kunufaika na hizo fursa; kwa ajili ya kuchakata au kushiriki katika mchakato wote wa uzalishaji na matumizi sahihi ya rasilimali kwa ajili ya maendeleo, kujiimarisha na kuongeza kipato halali.

"Hayo mambo ni lazima uyafikirie vizuri, nyie mnaotaka kugombea au wagombea watarajiwa. Kwa hivyo, ninyi ambao mmeonyesha nia lazima muangalie," alisema.



Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Salim Msangi (wa pili kulia), alipotembelea banda la mamlaka hiyo, katika Mkutano wa 17 wa Wadau wa Sekta ya Uchukuzi kuhusu Ufuatiliaji na Tathmini, jijini Arusha juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mhagama ataka tathmini ya kina hali ya utapiamlo kwa halmashauri

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Afya, Jenista Mhagama, ameagiza halmashauri zote nchini, kufanya tathmini ya kina ya hali ya lishe ili kubaini matatizo ya utapiamlo kwa kila halmashauri.

Ameagiza tathimini hiyo ifanywe sambamba na utekelezaji wa afua za lishe na uongezaji wa virutubishi kwenye vyakula.

Mhagana alitoa agizo hilo jna jijini hapa wakati akitoa taarifa kuhusu maadhimisho ya Siku ya Lishe kitaifa yaliyotanguliwa na kaulimbiu 'Mchongo Ni Afya Yako, Zingatia Unachokula.'

Alisema endapo kila halmashauri zikitenga fedha zitawezesha kusaidia jamii kupata elimu na uelewa zaidi ngazi ya kata na shuleni ili kupunguza utapiamlo na kupata jamii bora kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

"Niwakumbushe watalaam wetu wa afya na lishe katika ngazi zote kuhakikisha kuwa kila mmoja kutoa elimu, ikiwsmo uhamasishaji jamii kuhusu ulaji unaofaa na matumizi ya vyakula vilivyoongezwa virutubishi kupitia majukwaa mbalimbali.

"Naziagiza halamshauri zote nchini kuhakikisha zinaimarisha usimamizi wa utekelezaji wa afua za lishe katika ngazi zote, ili kuhakikisha afua hizi muhimu zinatekelezwa kwa ufanisi na kwa kuzingatia sera, miongozo, kanuni na taratibu zilizopo," alisema.

Pia alisema jamii bado inakabiliwa na utapiamlo wa aina nyingi, zikiwamo ukondefu, udumavu, uzito pungufu hususan kwa watoto,upungufu wa vitamini na madini mwilini, yaani njaa iliyofichika, upungufu wa damu, lishe ya kuzidi, kiribatumbo na magonjwa yasiyoambukiza. "Utapiamlo hudhoofisha makuzi ya watoto kimwili na kiakili ikiwamo kuongeza hatari ya magonjwa na kutuletea gharama kubwa za matibabu kwani serikali inatenga Sh. bilioni tano kila mwaka katika taasisi za afya kwa ajali ya kupambana na magonjwa yasiyoambukiza yakiwamo sukari, figo, moyo na shinikizo la damu," alisema.

Pia alisema utapiamlo hudhoofisha makuzi ya watoto kimwili na kiakili, kuongeza hatari ya magonjwa na kukosa ubunifu, uwezo wa kufanya maamuzi wakati wa utu uzima, hivyo ni vizuri kuchukua hatua za makusudi kwa kufanya uamuzi sahihi kila siku ya kula aina bora za vyakula na kufanya mazoezi.

Aidha, alitoa tahadhari kwa jamii kupunguza hatari ya kupata utapiamlo wa lishe ya kuzidi na magonjwa yasiyoambukizi katika jamii, kama vile kisukari,shinikizo la juu la damu, magonjwa ya moyo,kiharusi na magonjwa ya figo.

Pia alisema ni muhimu kushirikiana na serikali kuhamasisha jamii ulaji unaofaa na matumizi ya vyakula vilivyoongezwa virutubishi kupitia majukwa mbalimbali.

"Niwakumbushe watalaam wetu wa Afya na Lishe katika ngazi zote kuhakikisha kuwa kila mmoja anatoa elimu ikiwemo uhamasishaji jamii kuhusu ulaji unaofaa na matumizi ya vyakula vilivyoongezwa virutubishi kupitia majukwaa mbalimbali ili kupunguza utapiamlo na viribatumbo," alisema

Alisema kwa mujibu wa takiwmu za Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), inaonyesha kila mwaka watoto 1,500 wanapatikana na matatizo ya moyo.

# Wapanda miti ya matunda shuleni ili kupata lishe

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

WANAFUNZI wa shule za msingi na sekondari za Jiji la Arusha, wameanza kutekeleza kwa vitendo, kampeni ya upandaji miti ya matunda kuzunguka viunga vya shule zao.

Kampeni hiyo ina lengo la kuchochea afua za lishe kuimarisha lishe bora itakayolisaidia taifa kuhimili changamoto ya utapiamlo kwa watoto. Kuanzishwa kwa kampeni hiyo, kunatokana na tatizo la lishe kuwa tishio nchini.

Akizungumza jana katika Shule ya Sekondari ya Kinana kuhusiana na kampeni hiyo inayoendeshwa na vijana walioamua kujiajiri katika mifumo ya chakula, Ofisa Vijana wa Gain Tanzania, Saddam Khalfan, alisema kampeni hiyo inalenga kuhamasisha wanafunzi kutambua umuhimu wa lishe.

Kampeni hiyo inaongozwa na Taasisi ya Arusha Food System Youth Leaders na Shirika la Global Alliance for Improved Nutrition (gain).

"Tumepanda miti ya matunda 500 katika shule za msingi na sekondari za jiji la Arusha, ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani na tunatoa elimu ya lishe kwa wanafunzi na vijana ili kutambua umuhimu wa lishe bora hasa katika kujenga mwili.

"Lengo kubwa ni kuhamasisha kundi la vijana na watoto waliopo shuleni, kutambua umuhimu wa upandaji miti ya matunda ambayo ni chanzo kikubwa cha lishe. Tunaamini upandaji miti ya matunda, utasaidia kupata lishe, kutunza mazingira na kuboresha mazingira ya shule na afya za wanafunzi. Hapa tunapanda miti 200 na shule zingine tutapanda miti 300," alisema.

Kabla ya kuanza kampeni hiyo, Ofisa Lishe wa Jiji la Arusha, Namsifu Godson, alisema upandaji wa miti ya matunda, utahamasisha jamii kuhusu lishe ambapo matunda na mboga ni miongoni mwa makundi muhimu.

Mmoja wa viongozi wa mfumo wa chakula kutoka Taasisi ya Arusha Food Systems Youth Leaders, Regina Mlay, alisema kwa mwaka huu wameadhimisha siku hiyo kwa namna tofauti kwa kupanda miti na kutoa elimu kwa vijana na wanafunzi.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kuendelea kuweka mkazo kwa jamii juu ya umuhimu wa lishe bora.

Kampeni hiyo ni sehemu ya Mradi wa Nourishing Food Pathway (NFP), unatekelekezwa na GAIN na unafadhiliwa na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU), Serikali ya Uholanzi, Serikali ya Uingereza na wadau wengine kutoka taasisi binafsi.

## TULIKOTOKA,TULIPO & TUNAKOKWENDA...




# Kwa nini nyimbo 'Georgina', 'Rangi ya Chungwa' hazichuji?

**Na Adam Fungamwango**

HADI leo hii mwaka 2024, ukienda kwenye bendi yoyote inayopiga muziki 'laivu', haitomaliza onyesho lake kabla hazijapigwa nyimbo mbili maarufu sana.

Ni 'Georgina' na 'Rangi ya Chungwa'. Hata kama wanamuziki wenyewe hawakuwa na mpango nazo kuzipiga, lakini yatapelekwa maombi jukwaani kutaka zipigwe.

Hao ni wapenzi wa muziki waliohudhuria onyesho, ndiyo huwa kwa kiasi kikubwa wakiomba nyimbo hizo zipigwe. Wapo kwenye umri mkubwa wanaoomba, lakini cha kushangazwa zinaombwa na vijana wenye umri hata wa miaka 20, wavulana kwa wasichana.

Kitakachokushangaza zaidi, nyimbo hizo zinapopigwa, vijana wenye umri wa kuanzia miaka 18 na 25, wanauimba kwa kufuatisha maneno vile vile, utafikiri ni nyimbo mpya zilizorekodiwa miaka ya hii ya 2000.

Mbali na kuimba mashairi yake neno kwa neno, lakini huimba kwa hisia kali, huku wakicheza na kuonyesha kabisaa si tu kwamba wanaburudika na muziki 'laivu' tu, lakini hata maudhui nyimbo hizo yanawaingia moyoni.

Ni kweli kuwa nyimbo nyingi za zamani za dansi zimeendelea kupendwa na mashabiki wengi wa muziki na hazipachika majina ya 'muziki usiokufa', lakini nyimbo hizi mbili ndizo zimekuwa kama vinara ya nyimbo zote za zamani kwa kupendwa.

'Georgina' na 'Rangi ya Chungwa' zilirekodiwa katikati ya miaka ya 1970 na mbili mbili mbalimbali ambazo hazikuwa kubwa sana, lakini nyimbo hizi zikawa maarufu zaidi kuliko hata bendi zenyewe.

Hata hawa vijana wa sasa ambao wanazipenda nyimbo hizi, pamoja na kuziimba kana kwamba ni za 'bongo fleva', lakini wengi hawajui zimepigwa bendi gani.

Sana, anaweza kutokea mmoja akasema Marijani Rajabu. Atakuwa yupo sahihi. Wimbo huu ulipigwa na bendi ya Safari Trippers, ukiimbwa na Marijani, lakini ulitungwa na Khalfan Uvuruge.

Kisa cha wimbo huu ni cha kweli, na msichana huyo Georgina alikuwepo. Ni kwamba wanamuziki bendi hiyo walipokuwa wakitoka mazoezini siku moja waliwenda kwenye nyumba moja wakagonga hodi wakaomba maji ya kunywa. Kumbuka zamani hakukuwepo maji ya chupa madukani na ulikuwa ni utaratibu wa kawaida zamani kwa mtu kuomba maji ya kunywa kwenye nyumba yoyote ile njiani hata kama huijui na hawakujui, lakini utapewa tu.

Msichana Georgina ndiye aliyewapa maji, na Uvuruge alivutiwa naye, uhusiano ukaanzia hapo.

Baba mtu akatonywa kuwa binti yake ambaye ni mwanafunzi wa sekondari wakati huo ana uhusiano na vijana wa bendi inayofanya mazoezi jirani ya nyumbani kwake.

Alichofanya mzee akamhamisha shule kumpeleka mikoani, ndipo Uvuruge alipotunga wimbo huo.

"Oooh Georgina, siku ulioyoondoka, uliniacha nalia na machozi, umekwenda kuishi mbali nami, Georgina ya mama. Sipati Usingizi nikikumbuka, tulivyoishi mimi nawe Georgina aa, ooh Georgina.

Umeondoka Georgina, umenichia masikitiko, Georgina Georgina oo." Ni baadhi tu maneno yaliyo kwenye wimbo huo.

Nyanyembe Jazz, si bendi inayojulikana na na wala waikuwa bendi kubwa wakati huo. Pia haina nyimbo nyingi maarufu. 'Rangi ya Chungwa' ndiyo wimbo wake maarufu zaidi kuliko bendi yenyewe hadi leo hii.

Awali uliitwa kwa jina la rangi ya kinywaji kimoja ambacho hadi leo kinauzwa madukani, na msichana aliyeimbwa alisifiwa kuwa ana rangi kama hiyo. Kamati ya Redio Tanzania (RTD), iliwaambia kama haina makubaliano ya kimkataba na wahusika na kampuni ya vinywaji wabadilishe. Ndipo walipobadilisha baadhi ya maneno, ikiwemo sasa kuwa 'Rangi ya Chungwa'.

**Tuma meseji 0716 350534**

# Kenya yapata naibu rais mpya

**NAIROBI, Kenya**

NAIBU rais mpya wa Kenya, Profesa Kithure Kindiki, ameapishwa rasmi na kuhitimisha rasmi zama za aliyeshika nafasi hiyo Rigathi Gachagua, ambaye aliondolewa madarakani.

Kindiki aliapishwa jana na kuwa naibu wa rais wa tatu baada ya Rigathi Gachagua kutimuliwa katikati ya mwezi Oktoba kwa makosa ya ufisadi, kukiuka katiba na matumizi mabaya ya madaraka.

Kuapishwa kwake kunatokana na jopo la majaji watatu kuondoa zuio lilowekwa awali na mahakama baada ya kufunguliwa kwa kesi ya kupinga kuondolewa madarakani Gachagua.

Profesa Kindiki amekula kiapo cha utekelezaji wa majukumu yake kwa uadilifu kama naibu rais.

Wakati akila kiapo, profesa Kindiki aliahidi kufanya kazi kwa uwezo wake wote na kusisitiza kuwa mtu yoyote anaweza kufikia nafasi yoyote katika maisha yake kwa uwezi wa mwenyezi Mungu, bila kujali Historia.

Msajili mkuu wa mahakama kuu, Winfrida Mokaya, akisaidiwa na Jaji mkuu Martha Koome aliongoza kiapo hicho kwa kufuata katiba ya nchi hiyo.

Shughuli hiyo ilianza rasmi saa tano kasoro dakika 18 kwenye viwanja vya jengo la mikutano la kimataifa la KICC lililoko katikati ya jiji la Nairobi.

Katika hafla hiyo, nyimbo za kitamaduni zilisikika kama shamrashamra za uapisho huo.

Aidha, kulikuwepo na ulinzi mkali katika maeneo yaliyo karibu na KICC.

Profesa Kindiki aliambatana na mkewe Dr Joyce Gatiria Kithure ambaye amekuwa akimuunga mkono kila wakati katika safari yake ya kisiasa.

Rais William Ruto aliwasiri katika viwanja hivyo akiwa na mkewe Rachel Ruto.

Katika hutuba yake, Rais Ruto,aliwaambia Wakenya kuwa nia yake ni kuwahudumia na sio kuendekeza ubinafsi na kuweka Imani kwa naibu rais huyo mpya atamsaidia.

"Naamini utakuwa msaidizi mwema kwangu kwani nimekuwa mpweke uongozini kwenye ofisi ya juu zaidi.Ninatumai yote yaliyonipita katika miaka miwili iliyopita utaweza kulijaza pengo." alisisitiza.

Hafla hii iliwaleta pamoja pia viongozi wa ngazi ya juu serikalini wakiwemo spika wa bunge la taifa na baraza la senate kadhalika mawaziri na mabalozi wa nchi za kigeni. Ifahamike kuwa leo imetengwa kuwa siku ya mapumziko.

Profesa Kithure Kindiki mwenye miaka 52 amekuwa mwandani wa rais kwa zaidi ya muongo mmoja tangu William Ruto alipokuwa mbunge wa Eldoret North.

Pia alikuwa mwanasheria wake wakati alipoandamwa na kesi dhidi ya uhalifu wa binadamu kwenye mahakama ya kimataifa ya uhalifu wa kivita (ICC), iliyoko The Hague, Uholanzi.

Mkazi wa Othaya, Genesis Ngunjiri, alisema anaamini mahakama iko sahihi kwa kuruhusu kuapishwa kwa kiongozi huyo.

"Kwa vile Kindiki anatokea eneo la Mlima Kenya basi hatuna wasiwasi, achape kazi tu."alieleza.

Kindiki alichaguliwa kuwa Seneta wa kaunti ya Tharaka Nithi katika uchaguzi wa mwaka 2012, nafasi aliyoishikilia hadi 2022.

Katika kipindi hicho alihudumu kama mwakilishi wa chama tawala katika baraza la Senate, naibu spika na alitupwa katika nafasi hiyo wakati rais mstaafu Uhuru Kenyatta alipokuwa akisafisha chama cha Jubilee.

**DW**



Rais wa Kenya William Ruto(kushoto) akimkabidhi katiba naibu rais mpya Profesa Kithure Kindiki, baada ya kuapishwa. **PICHA: AP**

# Chama tawala Botswana chaondolewa madarakani

**GABORONE, Botswana**

CHAMA tawala nchini Botswana, kimeondolewa madarakani baada ya mgombea wa upinzani kushinda katika uchaguzi mkuu.

Chama cha Botswana Democratic Part (BDP) kimekuwa madarakani tangu nchi hiyo kupata uhuru mwaka 1966, kilikuwa kimeshinda kiti kimoja pekee cha ubunge kufikia mapema Ijumaa asubuhi, matokeo ya awali ya uchaguzi yanaonesha.

Chama cha Umbrella for Democratic Change (UDC), kinachoongozwa na wakili, Duma Boko, kilishinda viti 20, kulingana na hesabu za awali.

UDC kinaonekana kitaunda serikali huku kikitarajiwa kupitisha kizingiti cha viti 31 kwa wingi wa wabunge.

Duma Boko yuko mbioni kuwa mkuu wa nchi mara bunge litakapokutana kwa mara ya kwanza.

Boko, ambaye anagombea kwa mara ya tatu, aliwataka wafuasi wake kuwa makini na wenye nidhamu.

Licha ya kusimamia mabadiliko nchini Botswana, lakini ukuaji wa uchumi unasuasua kutokana na ukosefu wa ajira na kusababisha kupungua kwa umaarufu wa BDP.

Boko atachukua nafasi ya Mokgweetsi Masisi ambaye aliingia madarakani 2018.

Katika kampeni yake Masisi alinadi ujumbe kwamba chama chake kinaweza kuleta mabadiliko, wapiga kura hawakuunga mkono.

**BBC**

# Hezbollah yaishambulia Israel na kuua saba

**TEL AVIV, Israel**

KUNDI la Hezbollah limefanya mashambulizi ya roketi kaskazini mwa Israel na kuua watu saba.

Tukio hilo limeelezwa kuwa ni baya tangu mapigano kati ya jeshi la Israel kufanya mashambulizi kusini mwa Lebanon.

Waziri wa Mambo ya Nje, Israel Ktz, alisema mashambulizi hayo yameua mkulima wa Israel na wafanyakazi wanne wa kigeni waliokuwa shambani wakati roketi zilipotua karibu na mji wa Metula, ambao uko kwenye mpaka na Lebanon.

Baadaye, mwanamke wa Kiisraeli na mtoto wake waliuawa katika shamba la mizeituni karibu na kijiji cha wa Kibbutz Afek, nje kidogo ya mji wa pwani wa Haifa. Hezbollah ilisema ilirusha makombora kuelekea eneo la Krayot kaskazini mwa Haifa na kwenye ngome ya vikosi vya Israel iliyopo kusini mwa mji wa Khiam ndani ya Lebanon.

Jeshi lilisema jumla ya makombora 55 yalirushwa kuelekea eneo la Magharibi mwa Galilaya, iliko miji ya kibbutz , Galilaya ya Kati na Galilaya ya Juu mapema jana alasiri. Baadhi ya makombora yalidunguliwa na mifumo ya ulinzi wa makombora ya ang awa Israel huku mengine yakaanguka katika maeneo ya wazi, liliongeza jeshi la Israel.

**BBC**



Mkuu wa kitengo cha Biashara Incubator kutoka Benki ya Stanbic Tanzania, Kai Mollel akizungumza wakati akifungua awamu ya saba ya Program ya Maendeleo ya Wasambazaji 'Supplier Development Program', jijini Dar es Salaam jana, iliyohusisha wanawake na vijana ambao ni wamiliki na waendeshaji wa biashara za chakula kwa lengo la kuwapa stadi na maarifa, kuwaunganisha na mitaji, masoko na kuongeza thamani ya uzalishaji wa biashara ya chakula kwenda viwango vya kimataifa kwa kualika watu mbalimbali na kuwapa elimu ya namna ya kufika hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PAC yataka TRA kukamilisha mifumo wa ukusanyaji mapato

**Na Jenifer Gilla**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imependekeza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kukamilisha maboresho ya ujenzi na usimikaji wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato.

Imesema hali hiyo itaiepusha serikali na changamoto ya kutofikia lengo la kukusanya mapato, hivyo kuipunguzia uwezo wa kutimiza majukumu yake.

Mapendekezo hayo yametokana na upungufu uliobainishwa na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na nakisi ya Sh. trilioni 1.069 ya mapato ambayo hayakukusanywa na TRA kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Joseph Kakunda, alisema juzi wakati akiwasilisha uchambuzi wa ripoti ya CAG ya hesabu zilizokaguliwa za serikali kuu na mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2023.

Alisema nakisi hiyo imetokana na upungufu mbalimbali ikiwamo changamoto za mifumo ya kodi, mizigo inayotakiwa kusafirishwa kwenda nje ya nchi na badala yake inatumika nchini bila kulipiwa kodi. Upungufu mwingine ni kutowasilishwa kwa wakati ritani za kodi kwa wakati na dosari katika ushughulikiaji wa mashauri ya kikodi.

"Kutofikiwa lengo la ukusanyaji wa mapato kunaikosesha serikali mapato stahiki na hivyo kupunguza uwezo wa serikali kuwa na rasilimali za kutosha kutimiza majukumu yake," alisema Kakunda.

Alisema kamati hiyo pia ilipendekeza TRA ikamilishe mchakato wa kutambua na kusajili idadi halisi ya walipakodi waliopo nchini na ihuishe kanzi data ya walipakodi, ili kuwezesha kutambua aina ya kodi na kiasi kinachotakiwa au kinaweza kukusanywa kutoka kwa walipakodi husika na kupata uhalisia wa mwenendo wa ukusanyaji wa kodi.

Vilevile alisema kamati ilipendekeza TANESCO iandae na kutekeleza kikamilifu mkakati na mpango wa malipo, ili kuhakikisha malipo ya deni la TPDC ya Sh. bilioni 713 yanafanyika kwa wakati ili kuepusha kuendelea kukua kwa deni hilo.

Alisema kuchelewa kulipwa kwa deni hilo kunaathari kubwa kwa fedha za umma kwa kuwa linasababisha ongezeko la malipo yanayotokana na riba kubwa hali inayoongeza changamoto ya madeni kwa TANESCO pia inaathiri hali ya kifedha na ukwasi ya TPDC hivyo kupunguza ufanisi wa kiutendaji kazi.

**HESLB IWE MFUKO**

Aidha, kamati hiyo pia iliishauri serikali kuangalia uwezekano wa kuifanya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kuwa mfuko ili kuipa uwezo wa kupata vyanzo vya ziada vya fedha ikiwamo kuwekeza kwa faida na kujenga uwezo stahimilivu kukopesha wanafunzi wengi wenye uhitaji ambao mahitaji yanaongezeka mwaka hadi mwaka;

Hali hiyo, kamati ilisema itasaidia kuondoa changamoto zilizoibuliwa na katika ripoti ya CAG ya mwaka 2022/23 kama vile bodi kutokidhi mahitaji ya kifedha kwa wahitaji wa mikopo kwa Sh. bilioni 198.9, baadhi ya wanafunzi kupewa mikopo isiyostahili na kutokusanywa kwa mikopo ya Sh. trilioni 2.2 ambayo imekwishatolewa hadi sasa.

Aidha, iliishauri serikali pamoja na mambo mengine ihakikishe wigo wa bajeti wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali unaongezeka, ili kuboresha mazingira ya kazi na ubora wa huduma zitolewazo na ofisi hiyo na iwajengee uwezo mawakili kwa kuwapatia mafunzo katika maeneo maalum ya kimkakati.

Iliishauri pia iweke utaratibu ambao utawezesha ofisi hiyo kushiriki kikamilifu katika hatua za awali za uingiaji na utekelezaji wa mikataba inayoingiwa na wizara, idara na taasisi za serikali, ili kuikinga serikali na hasara zinazotokana na serikali kushtakiwa kwenye kesi za madai na ihakikishe masuala ya uwekezaji yanasimamiwa ipasavyo kwa mujibu wa sheria na mikataba inayokuwa imeingiwa ili kuepusha madai makubwa kwenye maeneo hayo.

Alisema mikakati hiyo itaisaidia serikali kujiepusha na changamoto zilizobainishwa katika ripoti ya CAG kama vile bajeti isiyotosheleza, gharama kubwa za uendeshaji na usimamizi wa mashauri ya usuluhishi na baadhi ya taasisi za serikali kutozingatia masharti ya uvunjaji wa mikataba waliyoingia.

Kamati hiyo pia ilipendekeza ifanye mapitio ya Mkataba wa Makubaliano uliongiwa kati ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na London School of Hygiene and Tropical Medicine (LSHTM), ili kuhakikisha yanazingatia Sheria mama ya NIMR na kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa.

Aidha, ilipendekeza pia NIMR ihakikishe hesabu za kila robo mwaka na za mwaka za Kituo cha Mwanza Intervention Trials Unit (MITU - Mwanza) zinaandaliwa na kupitiwa kwa pamoja kisha ziwasilishwe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa ukaguzi.

Kakunda alisema bunge liliazimia kuwa kabla ya kukamilika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Fedha na Wizara ya Maji ziandae na kutekeleza mkakati wa uwajibikaji utakaowezesha ufuatiliaji wa malipo ya Taasisi za Umma kwa Mamlaka za Maji inazozidai taasisi za umma.

Alisema mkakati huo utasaidia kupata suluhisho la kudumu litakalohakikisha kuwa huduma za maji zinaendelea kutolewa bila kutatizwa na madeni ya taasisi za serikali.

# Angalizo latolewa ufugaji wa kuku katika vizimba

**Na Beatrice Shayo**

WAFUGAJI wa kuku nchini, hasa wanaotumia vizimba, wameshauriwa kuzingatia haki za ustawi wa wanyama wanapowafuga ili wapate soko ndani na nje ya nchi.

Ushauri huo ulitolewa Juzi na Mkurugenzi Msaidizi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Aneth Kitambi, wakati wa mafunzo yaliyolenga kuzingatia haki za wanyama kwa upande wa kuku na ndege wengine ambao wanafugwa.

"Tulikuwa tunaangalia madhara ya kuku kufugwa kwenye vizimba (Cages). Cages zipo za aina mbalimbali tumeona wakifugwa wengi sehemu moja wanaathirika kwa sababu hawazingatii ukubwa wa eneo na kusababisha madhara katika uzalishaji," alisema.

Alisema kuku aliyefugwa kwa vizimba thamani yake katika soko inauzwa bei ya chini ikilinganishwa na wengine wanaofugwa katika eneo kubwa wanajiachia na wanaweza kuruka na hata nyama yake huwa ina ladha nzuri.

Dk. Kitambi alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wafugaji kuendelea kufuga kwa kuzingatia ustawi wa wanyama ili wapate soko kwa wingi.

Aidha, alisema kuna maazimio waliyokubaliana ya muda mfupi na muda mrefu lengo kubwa ni kuhakikisha wafugaji wanazingatia haki za wanyama ikiwamo kuku na ndege wengine wanaofugwa.

Alisema sera na kanuni zao zipo vizuri ingawa kuna vipengele vichache ambavyo wanaendelea kuviongeza ili kuboresha sekta hiyo kwa kuwa masoko mengi yanataka kuzingatia haki za wanyama hao.

Aidha, alisema wataendelea kuwasiliana na balozi mbalimbali ili kupata masoko ambayo yanahitaji bidhaa zinazotokana na kuku wanaofugwa nje ya vizimba.

Alisema kwa Tanzania ufugaji wa vizimba bado ni mchache ni kati ya asilimia 10 hadi 20, hivyo kuku wengi wanafugwa kwenye maeneo mapana ndio maana watu wanapenda hiyo bidhaa.

"Rekebisho moja wapo ni kuhakikisha kuku wanaofugwa kwenye vizimba wanapunguza idadi na kuweka uwiano unaotakiwa badala ya kuwajaza wengi kwenye vizimba kufanya hivyo ni kuwanyima haki zao," alisema.

Mratibu wa Kituo cha elimu na ustawi wa wanyama kilichoko mkoani Dodoma, Ayubu Nnko, alisema kuna changamoto kubwa ya ufugaji wa kuku kwa kutumia vizimba kwa kuwa hawana uhuru hata wa kuruka na usalama wao upo hatarini.

Alisema wafugaji wengi wanakimbilia kufuga kwenye vizimba ili kurahisisha ufugaji bila kujali haki za ustawi wa wanyama hao.

"Kwenye hao kuku wa vizimba kunakuwa na magonjwa yanayosababishwa na mfumo wa hewa. Wafugaji wengi wanaofuga kwenye cage usafi wao ni duni jambo hilo serikali ilitizame kwa umakini," alisema.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.
Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile.
Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-37

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Akatoa simu yake na kibonyeza kitufe na maneno ikasikika sauti yake siku ambayo aliongea na mpenzi wake jinsi alivyopokea vitisho kwa watu asiowajua.

"Mariamu mchumba wangu, nyota nadhifu wa moyo wangu, naomba unikubalie hili nitakalokuomba, kama ulivyonikubalia tukawa sote.

Kwa sasa najijutia mpenzi, nimejitosa ndani ya moto na matatizo, kuwa na wewe imekuwa nongwa, kwao ni kero kwa wasiopenda niwe na wewe."

Mariamu, wewe ni mrembo, Mungu hakukubakisha kitu, ni mzuri, mrembo una umbile zuri, lakini uzuri wako na ufukara kwao ni vibaya, roho zinawauma."

Ninachokuomba sasa Mariamu, imenibidi, ni bora nilivue mimi hili penzi, niwape nafasi waoamini umeshushwa kwa ajili yao si vyema uwe na mimi."

"Ingawa tumeapa kutotengena nawe mpaka kifo kabla hata hatujafunga ndoa, lakini inatubidi tutengane, niwaridhishe wale wabaya kwenye pendo letu."

Klipu ilimalizika na kuanza kuwaliza akinamama wengi mahakamani hapo baada ya kuisikia.

Kuwabembeleza haikuwezekana, badala yake majaji waliamua waiahirishe kesi hiyo hadi siku nyingine.

Maneno hayo ndiyo yaliyochukua kichwa vya habari kesho yake kwenye magazeti na kutamkwa kwenye televisheni na mitandao ya kijamii.

Yaliendelea kuwahuzunisha wengi kuona kumbe hata kabla Mariamu hajauawa mpenzi wake alipata vitisho vilivyomfanya atake kumuacha. Sasa kwa nini hakumuacha? Kwa nini aliendelea naye? Kwa nini badala ya kuuawa mwanaume, akauawa Mariamu? Hilo lingejulikana kama kusingekuwa na vilio mahakamani kiasi cha majaji kuahirisha kesi hiyo yenye mvuto.

*******************************************

Kutokana na mvuto mkubwa wa kesi hiyo, ilipangwa kuendelea baada ya siku tatu tu. Jinsi kesi yenyewe ilivyokuwa na mvuto kwenye jamii, ushahidi ulivyoanza kutolewa na kuripotiwa kwenye vyombo ya habari kama redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii, ilizidi kuitikisa nchi.

Siku ya kesi watu walijazana mara tatu kuliko ya kwanza. Ilibidi watu muhimu tu wakiwemo ndugu wa karibu wa pande zote mbili ndiyo waingie ndani. Wengine walibaki nje. Kilichoamriwa ni kuwekwa kwa spika nje ili watu waweze kusikia kinachozungumza kutokana na unyeti wa kesi hiyo.




**"Mtoto wa watu hana kosa, unataka kumuua kwa sababu gani, kwa sababu ya pesa zako, utajiri wako, kumbuka ukifanya hivyo tu, nakwenda kukuripoti polisi, halafu na mimi najiua. Siwezi kuona mtoto wa watu ameuawa kwa sababu yangu, halafu mimi nikaendelea kula raha duniani. Kama huko kuna kuoana, basi tukakwenda kuoana paradiso."**

Mtoa ushahidi upande wa mashtaka Kamal alikuwa akiendelea kutoa ushahidi wake ambao ulikatishwa kutokana na vilio vya watu, hususan akinamama.

Meseji aliyoisoma hapo ambayo alimwambia mchumba wake ambaye kwa sasa ni marehemu kuwa waachane kutokana na kupata vitisho iliwaliza wengi.

Baada ya hapo alitoa simu ya marehemu Mariamu. Ilipokaguliwa kisheria ilikubalika kuwa ni simu yake kweli.

Kamal alisema aliigundua meseji kwenye simu ya marehemu mchumba wake kutoka kwenye namba tofauti zisizosajiliwa ambazo zilionekana kumtongoza na kumwambia yeye ni msichana mzuri hawezi kuishi na kapuku.

Na baada ya kuona kama hawatofanikiwa, wakatishia kuwa watamuua bwana yake ili tuone ataringia nini tena.

Meseji zile zilionyesha kuwa watu hao watamuua Kamal, ili kupata urahisi wa kumpata.

Baada ya hapo kulikuwa na meseji ambazo marehemu Mariamu alikuwa anamjibu au kuwajibu waliokuwa wanamtongoza.

"Mtoto wa watu hana kosa, unataka kumuua kwa sababu gani, kwa sababu ya pesa zako, utajiri wako, kumbuka ukifanya hivyo tu, nakwenda kukuripoti polisi, halafu na mimi najiua. Siwezi kuona mtoto wa watu ameuawa kwa sababu yangu, halafu mimi nikaendelea kula raha duniani. Kama huko kuna kuoana, basi tukakwenda kuoana paradiso."

Kamal aliendelea kusema kuwa meseji hizo aliziona baada ya mchumba wake kufariki na kwa hali ya kawaida asingeweza kumuonyesha wakati yupo hai, hivyo Mariamu alisimama imara na aliuawa kwa sababu yake.

"Msimamo wake wa kutaka kuwa na mimi badala ya huyo tajiri aliyezungumza ndiyo uliosababisha auawe na kudaiwa kuwa ameanguka mwenyewe wakati anafanya mazoezi.

Shahidi mmoja ambaye awali hakuwepo kwenye kesi hiyo, lakini aliamua kuja mwenyewe akidai ana kitu muhimu alipanda na kusema kuwa aliwaona washtakiwa wawili kati ya hao kwenye tukio la kumpiga au kumuua Mariamu.

Awali kijana huyo aliogopa baada ya kuona kuna upindishwaji wa taarifa, hivyo akaamua kujikalia kimya lakini akiwa na kitu moyoni mwake.

Baada ya kuona wahusika ambao hata yeye aliwaona wamefanya hivyo, akaamua kwenda kutaka kuunganishwa kutoa ushahidi.

Bakari Pusi, kijana na miaka 22, alisema aliwaona wahuhumiwa wawili kwa macho yake wakimbeba marehemu na kumpakiza kwenye gari haraka haraka, tukio ambalo halikuonwa na watu wengi kuanzia mwanzo hadi mwisho, hivyo kushindwa kuunganisha matukio.

"Siku hiyo nilikuwa natoka kwa rafiki yangu, mapema tu saa mbili hivi, nikapishana na jamaa mmoja ambaye aliniangalia machoni na mimi nikamuangalia. Tukapishana. Mimi nikaenda mbele, lakini kuna kitu nikawa nimesahau. Wakati narudi ile kukata kona, nikamuona yule jamaa ametoa kitu kama chuma hivi akampiga nacho dada mmoja kichogoni. Alikuwa anatoka nyumbani wake, alikuwa amemalizika kufunga kigeti cha nje ya mlango wake. Yule mdada akaanguka chini. Haraka akatokea mtu mwingine aliyetokea upande mwingine, wakambeba haraka sana. Mimi nilijibanza sehemu ili wasinione. Nikanyata na kuwafuatilia. Nikawaona wanamuingiza kwenye gari. Kusema ukweli sikuweza kufahamu kama walimuua pale pale, au alikufa baadaye.

Sikumwambia mtu lile tukio kwa sababu lilikuwa ni la kutisha na kuogofya, pia niliogopa kuisaidia polisi maana ingeonekana mimi nimeliona lakini hakuna mtuhumiwa aliyekamatwa.

Kesho yake tukasikia yule mdada ambaye mimi namfahamu amefariki kwa kuanguka kwenye mtaro mmoja wakati anafanya mazoezi kwa mshtuko wa moyo, nilishangaa sana, lakini ilikuwa ni siri yangu.

Baada ya wananchi na ndugu kukataa ripoti nilidhani kuwa italetwa ya tukio ambalo linalifahamu, lakini ikasemwa kuwa mchumba wake Kamal ndiyo kamuua.

Haikuwa kweli, mimi mchumba wake namfahamu sana, huwa anafika mara kwa mara pale. Na aliyempiga na chuma namfahamu ni huyo hapo mheshimiwa jaji, aliyekuja kumsaidia kubeba huyo hapo mwingine, wote niliwakariri kabisa. Waliobaki kusema kweli mimi siwajui." Ulikuwa ushahidi wa Bakari.

Baada ya kupokea ushahidi huo, mahakama iliutaka ushahidi wa daktari Dancun Shija.

Mbali na kuwa ni mmoja wa madaktari waliofanya uchunguzi wa ripoti ya pili ambayo jumba bovu lilimuangukia Kamal kuonekana muuaji, lakini ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza kuonana na Kamal alikuwa amejificha kwenye hospitali yake binafsi pale Ilala ili asikamatwe.

Alijifanya mgonjwa ili alale pale kwa siku kadhaa, lakini lengo lilikuwa ni kukimbia kukamatwa na kupumzisha kichwa kutokana na kuamini kuwa sehemu pekee ambayo askari huwa hawatafuti wahalifu au watuhumiwa ni hospitali. Labda mtu huyo awe mpelelezi mzoefu na mbobezi, tena aliyepata taarifa za kiitelejensia.

***Itaendelea Jumamosi***

HABARI MICHEZO

# Singida BS waipigia hesabu kali Coastal

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Msaidizi wa Singida Black Stars, Denis Kitambi, amesema kikosi chake kiko tayari kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar.

Singida Black Stars itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kufungwa bao 1-0 na mabingwa watetezi, Yanga katika mechi iliyopita.

Kitambi alisema wamejiandaa kuingia kwa kwa tahadhari katika mechi hiyo kwa sababu wanakutana na moja ya timu imara.

Alisema licha ya kutumia nguvu nyingi katika mechi iliyopita dhidi ya Yanga, wameendelea kuboresha kikosi chake kwa kufanyia kazi makosa waliyoyafanya.

"Ukiangalia namba walivyocheza mechi zao mbili zilizopita, unaona wako imara na wanajua kucheza dhidi ya timu kubwa, na ukiangalia tofauti ya siku kati ya mechi dhidi ya Yanga na hii ya kesho (leo), ni siku mbili, tunarejesha nguvu za wachezaji wetu," Kitambi alisema.

Aliongeza wanawaheshimu Coastal Union kwa sababu wanajua wana kikosi chenye wachezaji wazoefu na wanaojua kupambana wakati wote.

"Wamecheza dhidi ya Simba wametoka sare 2-2, wamecheza dhidi ya Yanga wamepoteza kwa bao 1-0, ukiwaangalia unaona wana mbinu wa kuzikabili timu kubwa, kwa maana hiyo lazima tuingine kwa tahadhari, kwa sababu wana uwezo wa kukabiliana na mpinzani yoyote," alisema kocha huyo.

Naye nyota wa timu hiyo, Elvis Rupia, alisema wachezaji wote wako tayari kupambana na Coastal Union na matokeo ya mchezo uliopita hayajawatoa kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Rupia alisema wanaifahamu vyema Coastal Union na wataingia kuwakabili kwa umakini kwa sababu wanajua nao wanahitaji kupata ushindi.

"Tupo tayari kwa mchezo wa kesho (leo), makosa tuliyofanya katika mechi iliyopita dhidi ya Yanga tumeshayarekebisha, tumeyafanyia kazi na hayatajirudia tena,' alisema Rupia.

Aliongeza ligi ni ngumu kwa sababu timu zote zimejiimarisha kufanya vyema na si kusindikiza.

# SIMBA QUEENS YATAMBA IKIWAFATA CEASIAA KESHO

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Simba Queens kitaondoka Dar es Salaam kesho ili kuelekea Iringa kwa ya mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), dhidi ya wenyeji Ceasiaa Queens itakayochezwa Jumanne kwenye Uwanja wa CCM Samora mkoani humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Simba Queens, Selemani Makanya, alisema wamefanya maandalizi mazuri kuelekea mchezo huo na wanaamini wanaenda kubeba pointi tatu muhimu.

Makanya alisema wametumia vyema mapumziko ya Kalenda ya Kimataifa na sasa wanaamini wataonyesha kiwango bora katika mechi zao zinazofuata za ligi hiyo.

"Tunaondoka Dar es Salaam Jumapili, kila kitu kuelekea maandalizi ya mchezo huo kiko vizuri, tunajua tunaenda katika mchezo mgumu, ,, alisema Makanya.

Meneja huyo aliongeza wanafahamu mechi hiyo haitakuwa rahisi kwa kila upande kwa sababu timu zote zina wachezaji wenye uzoefu na ligi hiyo.

"Kila mechi kwetu sawa na fainali, tunajua kila timu imejiimarisha kusaka ushindi, hakuna mechi rahisi iwe nyumbani au ugenini, sera yetu ni ile ile, kila mechi ni sawa na fainali. Simba Queens imetumia vyema mapumziko ya ligi, lengo ni kuwa bora katika kila idara, tunajua hakuna mechi rahisi," Makanya alisema.

Aliongeza kipa wao chaguo la kwanza, Caroline Rufa, bado anaendelea na matibabu na nafasi yake ya kurejea kikosi kwa sasa bado.

"Kiukweli tunaumia kumkosa Caro, atakuwa nje kwa miezi tisa, ni kama vile tutamkosa msimu karibu wote," aliongeza meneja huyo.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Mussa Hassan ‚Mgosi' alisema Ligi Kuu ya Wanawake inaendelea kuimarika hivyo kila mechi inayochezwa inatarajiwa kuwa ngumu.

„Ligi ya msimu huu ni ngumu na sababu kubwa kila timu ilifanya usajili mzuri, mbio za ubingwa ni ngumu pia, na hakuna ambaye anataka kushuka daraja kirahisi," Mgosi alisema.

Aliongeza wamejiandaa kuonyesha kizuri katika kila mechi kwa sababu malengo yao ni kutetea ubingwa wa ligi hiyo yapo pale pale.

"Tunahitaji kurudi tena katika mashindano ya CECAFA (Afrika Mashariki na Kati), ni lazima tuwe mabingwa, tunataka kurekebisha tulipokosea ili msimu ujao tukafanye vizuri katika michuano hiyo ya kimataifa," Mgosi alisema.

Mechi nyingine za Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania zitakazochezwa Jumanne ni kati ya Yanga Princess dhidi ya Mashujaa Queens wakati JKT Queens itawaalika Mlandizi Queens huku Bunda Queens itawafuata Gets Program na Fountain Gate Girls itawakaribisha Alliance Girls.

Simba Queens yenye pointi sita ndio mabingwa watetezi na vinara wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania yenye timu 10 kutoka mikoa mbalimbali.




Kipa wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Aishi Manula akifanya mazoezi ya kujiandaa kuikaribisha Sudan katika mechi ya marudiano ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# Uchaguzi MZFA kufanyika leo

**Na Mwandishi Wetu**

UCHAGUZI Mkuu wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Mkoa wa Mwanza (MZFA), unatarajia kufanyika leo jijini humo, imeelezwa.

Maandalizi ya uchaguzi huo yamekamilika na viongozi watakaochaguliwa leo watakaa madarakani kwa muda wa miaka minne.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya MZFA, Wakili Mussa Nyamwelo, wanaowania nafasi ya uenyekiti ni Vedastus Lufano na Frank Deogratius.

Alisema nafasi ya Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), inawaniwa na mgombea mmoja ambaye ni Kelvin Patrick na wanaowania ujumbe wa Kamati ya Utendaji ya MZFA ni Almasi Almasi na Jackson Mapera.

"Tunatarajia kila kitu kitakwenda vizuri, uchaguzi huu utafanyika kwa kufuata kanuni za uchaguzi na si tofauti na hapo, tunatarajia wajumbe watatimiza majukumu yao vizuri," alisema Nyamwelo.

Kwa mujibu wa katiba mpya, Makamu Mwenyekiti atateuliwa na kupata baraka za wajumbe wa mkutano mkuu wakati Katibu mteule atapitishwa na Kamati ya Utendaji itakayoingia madarakani.

Tayari Dar es Salaam, Morogoro, Mtwara, Kagera, Lindi, Arusha, Simiyu, Kigoma, Dodoma, Singida, Katavi na Rukwa zimeshafanya uchaguzi, ikiwa ni maandalizi ya kuelekea uchaguzi wa TFF utakaofanyika mwakani.

## ZISIKUPITE

### CHILWELL KUONDOKA CHELSEA
KLABU ya West Ham inaweza kumnunua beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya England, Ben Chilwell, mwenye umri wa miaka 27 kutoka Chelsea katika dirisha dogo la usajili la Januari. ***(Inside Track podcast, via Team talk)***

### BAYERN YAMTAKA MUSIALA
KUONGEZA mkataba wa kiungo mkabaji, Jamal Musiala, mwenye umri wa miaka 21, ambao unadumu hadi 2026, ni kipaumbele kwa vigogo wa Ujerumani, Bayern Munich. ***(Bild)***

### SAHIN KUBAKIA DORTMUND
KLABU ya Borussia Dortmund kwa sasa haina mpango wa kuchukua nafasi ya Nuri Şahin kama kocha licha ya timu hiyo kuwa katika nafasi ya saba kwenye msimamo wa Bundesliga kufuatia kufungwa na Augsburg hapo Jumamosi iliyopita. ***(Sky Germany)***

### GUEHI MAMBO MAGUMU
CRYSTAL Palace inasitasita kuanzisha tena mazungumzo na Newcastle United kuhusu mlinzi wa England, Marc Guehi, mwenye umri wa miaka 24, wakati wa dirisha la usajili Januari. ***(Football Insider)***

### LUCCA ATAKIWA JUVE
JUVENTUS iko tayari kufanya mazungumzo mapya na Udinese kuhusu mpango wa kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Italia, Lorenzo Lucca, mwenye umri wa miaka 24. ***(Rudy Galetti)***

### BARCA, RAPHINHA KUTETA
BARCELONA wanaamini mkataba mpya na winga wa Brazil, Raphinha, utafanyika. Mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 utaendelea hadi mwaka, 2027. ***(Diario Sport)***

### PEDRI KUULA BARCA
MAJADILIANO kuhusu mkataba mpya kati wa kiungo wa kati wa Barca na Timu ya Taifa ya Hispania, Pedri, ambaye ana umri wa umri wa miaka 21, yanaendelea vyema. ***(Fabrizio Romano)***

### COSTA ATAKIWA BARCA
BARCELONA wameonyesha nia ya kumsajili mlinda mlango wa Porto ya Ureno, Diogo Costa, mwenye umri wa miaka 25, ambaye pia anasakwa na Manchester City, lakini kitita cha kumsajili kilichoongezeka hadi euro milioni 45 kinafanya dili kuwa gumu. ***(Sport)***

### SEMENYO AWEKWA SOKONI
FOWADI wa Ghana, Antoine Semenyo, alitia saini kuongeza mkataba mpya msimu wa joto lakini Newcastle United na Tottenham Hotspur zinazomwinda huenda zikaona ofa ya Bournemouth kwa mchezaji huyo wa miaka 24 kama mpango mwingine wa kumbakisha katika klabu hiyo. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# AMORIM AKUBALI KUHAMIA UNITED

●●● Kocha huyo mpya ataanza rasmi kibarua Novemba 24 kwa sababu...

**MANCHESTER, England**

RUBEN Amorim anatarajiwa kuanza kuinoa Manchester United wakati wa mapumziko ya kimataifa ya Novemba hii, vyanzo vilithibitisha kwa ESPN.

United na mabingwa wa Ligi Kuu Ureno, Sporting CP, wamefikia makubaliano ya kumchukua kocha huyo wiki hii.

Amorim anatarajiwa kurithi mikoba ya Erik ten Hag, ambaye alitimuliwa Jumatatu iliyopita, kama kocha mkuu wa Old Trafford na atakuwa uteuzi wa sita wa kudumu katika nafasi hiyo tangu kustaafu kwa Sir, Alex Ferguson mwaka, 2013.

Vyanzo viliiambia ESPN, United walitumia kifungu cha kutolewa cha kocha huyo wa zamani wa Braga cha euro milioni 10 huko Sporting, na klabu hiyo ya England pia italipa fidia ili kuwezesha idadi ya wafanyakazi wa Amorim kuungana naye Old Trafford.

Lakini kwa masharti ya mkataba wa Amorim katika klabu ya Sporting ikiwa ni pamoja na muda wa notisi ya siku 30, vyanzo vimeiambia ESPN, United italazimika kusubiri hadi katikati ya Novemba kwa Amorim kuchukua jukumu la kuinoa timu hiyo kufuatia mechi ya ugenini kati ya Sporting dhidi ya Braga itakayochezwa Novemba 10, mwaka huu.

Vyanzo vya ESPN vilisema, Ruud van Nistelrooy, ambaye aliiongoza United kushinda mabao 5-2 katika mechi ya raundi ya nne ya Kombe la Carabao dhidi ya Leicester City katika mchezo wake wa kwanza kama kocha mkuu wa muda Jumatano iliyopita, atasimamia michezo mitatu ijayo ya timu hiyo, ambayo itakuwa dhidi ya Chelsea, PAOK Thessaloniki na Leicester kabla ya kukabidhi mikoba kwa Amorim.

Mechi ya kwanza ya Amorim kuongoza itakuwa ya Ligi Kuu England dhidi ya Ipswich Town itakayofanyika Novemba 24, mwaka huu kwenye Uwanja wa Portman Road.

United iko katika nafasi ya 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England wakiwa wameshinda mechi tatu pekee kati ya tisa za mwanzo.



# Guardiola alia na majeruhi

**MANCHESTER, England**

KOCHA Mkuu wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu England, Manchester City, Pep Guardiola, amesema wingi wa majeruhi katika timu yake unampa wakati mgumu kwa sasa na inamlazimu kufanya mzunguko wa kikosi kutokana na wingi wa mechi.

Guardiola amesema Manchester City ina wachezaji 13 pekee walio kamili kucheza jambo ambalo linalomtatiza zaidi kwa sasa.

„Ndio, tuna wachezaji 13 tu walio tayari kucheza, wengi wao waliocheza hivi majuzi walimaliza na matatizo.

„Nadhani tuko katika kipindi kigumu sana kwa sababu kwa miaka tisa hatujawahi kuwa na majeruhi wengi hivi," alisema Guardiola.

City wameondoshwa katika michuano ya Kombe la Carabao kwa kupoteza kwa mabao 2-1 dhidi ya Tottenham Hotspur waliokuwa nyumbani.

# Ranieri ataka timu ya taifa



**ROME, Italia**

KOCHA wa zamani wa Leicester City, Claudio Ranieri, aliyetangaza kustaafu huenda akarejea uwanjani baada ya kutangaza atarudi kazini kama atapata nafasi katika timu ya taifa.

Ranieri alijizolea umaarufu mkubwa baada ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England mwaka 2016.

Pia amewahi kuzinoa klabu za Chelsea, Juventus, Atletico Madrid, Inter Milan na Monaco kabla ya kutangaza kustaafu Mei, mwaka huu.

„Ni kweli natamani kurejea tena kwenye kazi ingawa nimekataa zaidi ya ofa moja," alisema.

„Wacha tuone kama simu itatoka kwenye timu ya taifa," alisema kocha huyo mwemye umri wa miaka 73 akiliambia gazeti la kila siku la Corriere della Sera la Italia.

Ranieri alikataa pia kazi ya kuinoa Italia, akisema kwa wakati ule alikuwa na imani kubwa na meneja wa sasa wa timu hiyo maarufu kwa jina la Azzurri, Luciano Spalletti.



# KLOPP: RAMOS HAKUWA BEKI BORA

**MUNICH, Ujerumani**

KOCHA wa zamani wa Liverpool, Jürgen Klopp, amemkosoa, Sergio Ramos, wakati akimjadili nyota huyo wa zamani wa Real Madrid katika podikasti na Toni Kroos.

Klopp alihoji ikiwa Ramos alikuwa „mtu mzuri" wakati akitafakari changamoto faulo yake kwa Mohamed Salah wakati wa mechi ya Fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ya mwaka 2018.

Salah aliondoka uwanjani akilia kutokana na jeraha la bega mapema katika kipindi cha kwanza baada ya kugongana na Ramos.

Pia alihusika katika pambano na mlinda mlango, Loris Karius, na kumfanya afanye makosa mawili wakati Madrid iliposhinda fainali kwa mabao 3-1.

Akizungumza katika podikasti ya Kroos, Klopp alisema: „Je, Sergio Ramos ni mtu mzuri kweli? Si mchezaji ninayempenda.

„Kitendo hicho kilikuwa cha kinyama. Bila shaka, hawezi kujua kinamsumbua bega, lakini sote tunajua alionyesha furaha sana.

„Singeweza kamwe kuelewa mawazo hayo, sikuwahi kuwa na wachezaji kama hao na, walipofanya hivyo, nilihakikisha wameondoka."

Kroos alimtetea Ramos, akisema alikuwa „mchezaji mwenza mzuri sana," kabla ya Klopp kuongeza: „Huenda asiwe mchezaji ninayempenda, lakini haijalishi.

„Siku zote nilifikiri mabeki wangu wa kati walikuwa wazuri vya kutosha kutojihusisha na vitendo kama hivyo."

Klopp, ambaye alishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Liverpool mwaka 2019, aliihama klabu hiyo msimu uliopita, kabla ya kuchukua nafasi ya mkuu wa soka duniani katika Kampumi ya Red Bull mwezi uliopita.

HABARI MICHEZO

# NAMUNGO YAIPA JEURI KMC, YAJIPANGA KUIVURUGA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Namungo katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi, Kocha Mkuu wa KMC, Abdihamid Moallin, ameitumia salamu Simba, akisema watakwenda kutoa ushindani watakapokutana keshokutwa.

Ushindi huo ni wa pili mfululizo kwa KMC baada ya pia kuifunga Prisons mabao 2-1, nyumbani kwake kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini, Mbeya.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo huo juzi, kocha huyo raia wa Somalia, alisema ushindi wa mechi mbili mfululizo unampa 'jeuri' ya kuamini watawapa 'tabu' Simba kutokana na kikosi chake kuendelea kuimarika.

"Tulipata nafasi nyingi hatukuzitumia, lakini tumepata ushindi wa bao moja ni muhimu kwetu, tunashangalia, lakini tunakwenda kujiandaa na mchezo mwingine mkubwa dhidi ya Simba, inabidi tuwe tayari kukabiliana nao, nadhani kwa sasa kikosi changu kipo imara kupambana na timu yoyote, tunaamini tutafanya vizuri pia dhidi yao," alisema Moallin.

Bao ya KMC katika mechi hiyo lilifungwa dakika ya pili na Rashid Chambo, ambapo matokeo hao yamewapandisha Kino Boys hadi nafasi ya sita katika msimamo wa ligi ikifikisha pointi 14 baada ya kucheza michezo 10.

Naye Kocha Mkuu wa Namungo, Juma Mgunda, alisema kuzubaa kwa wachezaji wake na kutokuwa na utayari wa miili yao mwanzoni mwa mchezo huo kuliwafanya wapoteze mechi hiyo.

"Tumefanya makosa ya kutokuwa na utayari katika dakika za mwanzoni, wenzetu wakatuadhibu, lakini hii ni changamoto kwangu lazima nirekebishe hili, naamini siku hadi siku kikosi kitazidi kubadilika.

Kwa sasa tunakwenda kujipanga ili kufanya vizuri zaidi katika mechi zinazokuja," alisema kocha huyo ambaye aliongoza timu yake kushinda bao 1-0 dhidi ya Pamba Jiji.



Wachezaji wa Yanga Princess wakifanya mazoezi kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya Mashujaa Queens ya Kigoma itakayochezwa Jumanne kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# Pamba Jiji yaiwaza Fountain

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Pamba Jiji FC kinatarajia kuondoka Dodoma kesho kuelekea Babati tayari kwa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya wenyeji Fountain Gate FC utakaochezwa Jumanne kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa mkoani Manyara.

Ofisa Habari wa Fountain Gate, Moses William, alisema waliamua kubakia Dodoma baada ya kupata taarifa ya kusogezwa mbele mchezo huo ambao awali ulitarajiwa kuchezwa leo.

Ofisa huyo alisema mabadiliko hayo yaliwaathiri wachezaji wao kwa sababu walifanya maandalizi ya muda mrefu ili kupata matokeo mazuri.

"Taarifa ya mchezo kusogezwa mbele tuliipata tukiwa njiani tukalazimika kuvunja safari na kurudi Dodoma kuendelea na mazoezi," alisema William.

Aliongeza licha ya kutofanya vyema katika michezo iliyopita malengo yao ni kupambana kuhakikisha hawashuki daraja kirahisi.

" Kila mchezaji ana morali ya hali ya juu, tunawaomba mashabiki wetu wasikatishwe tamaa na matokeo yaliyopita, badala yake waendelee kutuunga mkono. Tunafahamu hatuna matokeo, hatujakata tamaa kwa sababu muda bado upo," aliongeza ofisa huyo.

## TFF : Taifa Stars imefuzu CHAN

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limesema hata kama Timu ya Taifa (Taifa Stars itafungwa na Sudan, itashiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), kwa sababu ni wenyeji wa michuano hiyo.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, amebainisha hayo baada ya mashabiki kuonekana kutoelewa nafasi ya Stars endapo itapata matokeo mabaya huku baadhi wakiuliza kwa nini Tanzania inacheza michezo ya kufuzu wakati ni mmoja kati ya wenyeji wa fainali hizo.

Ndimbo alisema kanuni zinaruhusu wenyeji wa michuano na fainali kucheza michezo ya kufuzu ili kuwafanya wapande viwango kama wakishinda na kuwekwa kwenye 'poti' la juu ili kupata timu rahisi za kucheza nazo.

"Hata kama hatutapata matokeo mbele ya Sudan bado tutacheza fainali hizo kwa sababu kwa mujibu ya utaratibu wenyeji wote watatu, Tanzania, Kenya na Uganda wote watakuwemo.

Kuna njia mbili ya kucheza fainali hizo, kuna kufuzu kwa uenyeji na kufuzu kwa nguvu za uwanjani, kizuri ni hata kama ni mwenyeji wa fainali au michuano, ukifuzu kwa kushinda uwanjani utakuwa na wakati mzuri wa kuwepo kwenye poti ambalo linaweza kukurahisishia kupata kundi ambalo halitakupa tabu, lakini ukifuzu kwa uenyeji tu huna chaguo unaweza kuwekwa poti lolote lile, hapo sasa unaweza kukumbana na kundi gumu," alisema Ndimbo.

Aliongeza wanauchukulia kwa umuhimu mkubwa mchezo wa kesho dhidi ya Sudan, utakaochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Katika mchezo wa kwanza uliochezwa, Oktoba 27, mwaka huu nchini Mauritania, Stars ilifungwa bao 1-0, ambapo sasa ina kazi moja tu ya kupata ushindi wowote ili kujiweka katika nafasi nzuri kuelekea fainali hizo za mwakani.


"Tuna matumaini ya kushinda mchezo huu kwa sababu sisi tunataka tufuzu kwa kupitia njia hii, na kumbukumbu zinaonyesha mara zote mbili tulizocheza fainali za CHAN kulipitia mgongo wa Sudan," alisema Ndimbo.

Mwaka 2019, Stars iliyokuwa chini ya Kocha Mkuu, Etienne Ndayiragije na Selemani Matola, iliwaondoa Sudan wakiwa nyumbani kwao na kufuzu kushiriki fainali za CHAN za mwaka huo.

Michezo
Jumamosi Novemba 2, 2024
Nipashe

## Klopp: Ramos hakuwa beki bora

UKURASA 22



# SIMBA SC YAIZIMA MASHUJAA KIGOMA

Bao la jioni la Mukwala lawapa pointi tatu muhimu na kuishusha...

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa kimataifa kutoka Uganda, Steven Mukwala, aliwapa furaha wanachama na mashabiki wa Simba, alipofunga bao pekee dakika za majeruhi dhidi ya Mashujaa FC katika mchezo mgumu wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani, Kigoma jana.

Ikiwa baadhi ya mashabiki wa Simba waliokuwa uwanjani na waliokuwa wanafuatilia mechi hiyo kupitia redio walijua mchezo huo ungeisha kwa suluhu, lakini mambo yalibadilika sekunde chache kabla ya kipenga cha mwisho.

Baada ya mwamuzi, Omari Mdoe, kuongeza dakika sita, zilicheza na ilipotimu dakika ya mwisho Simba ilipata kona mbili mfululizo ambazo zote zilipigwa na Awesu Awesu aliyeingia kipindi cha pili, moja ikiokolewa na ya pili ikizaa bao lililowapa Wekundu wa Msimbazi pointi tatu muhimu.

Mukwala aliingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Fabrice Ngoma, aliruka juu zaidi ya wachezaji wote na kuunganisha kwa kichwa mpira wa kona na kutinga wavuni na kuwaacha wachezaji wa Mashujaa, benchi la ufundi na mashabiki wao wasiamini kilichotokea.

Ni bao la pili kwa straika huyo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, moja akilifunga Agosti 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, Simba ilipocheza dhidi ya Fountain Gate na kupata ushindi wa mabao 4-0.

Ushindi wa jana umeipekeleka Simba hadi nafasi ya pili ikifikisha pointi 22 baada ya kucheza michezo tisa, ikishinda saba, sare moja na kupoteza mmoja, ikipachika mabao 17 na kuruhusu matatu.

Imeishusha Singida Black Stars yenye pointi 22 hadi nafasi ya tatu, ikiathiriwa na kufunga mabao 13 ambayo ni machache kuliko Simba.

Dakika ya pili tu ya mchezo, Leonel Ateba alianza kulisabahi lango la Mashujaa, lakini shuti lake la mguu wa kushoto lilipaa juu.

Mashujaa ilijibu shambulizi hilo dakika sita baadaye pale, Yusuph Dunia alipoambaa kwenye wingi ya kulia na kupiga krosi iliyoleta kizaazaa katika lango la Simba kabla ya Shomari Kapombe kuamua kuutoa mpira nje na kuwa kona.

Faulo ya moja kwa moja ya Kibu Denis nje ya eneo la hatari dakika ya 11, ilipanguliwa na kipa wa Mashujaa, Erick Johora na kuwa kona ambayo pia ilileta hatari tena, Kibu kwa mara ya pili alikaribia kufunga kwa kichwa, lakini mpira huo aliounganisha kwa kichwa ukapaa juu ya lango.



Mshambuliaji wa Simba, Leonel Ateba (kushoto), akijipanga kumtoka beki wa kati wa Mashujaa, AbdulMalik Gamal (aliyelala), katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani, Kigoma jana. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: SIMBA SC**

Dakika tisa baadaye Simba ilirejea tena kwenye lango la Mashujaa ambapo kama wachezaji wake, Ngoma, Kibu na Ladack Chasambi wangetulia wangeweza kuipatia timu yao mabao.

Ilikuwa ni krosi ya mguu wa kushoto ya Ateba, ambayo ilizua patashika nguo kuchanika langoni mwa Mashujaa, lakini wachezaji hao hawakuitendea haki.

Joshua Mutale ambaye alikuwa katika kiwango cha juu jana, aliwapiga chenga mabeki wa Mashujaa dakika ya 34 kabla ya kuachia shuti ambalo lilitoka pembeni mwa lango.

Kipindi chote cha kwanza, Simba ilitawala mpira kwa kiasi kikubwa, lakini Mashujaa walionekana kuweka viungo wakabaji wengi katikati ambao walivuruga mipango ya Simba, pia hawakuwaacha wapinzani wao wawe na utulivu pale wanapopata mpira.

Kipindi cha pili Mashujaa FC waliamua kukaa nyuma kulinda lango lao na walitumia muda mrefu kuokoa, kupiga mipira mirefu wakishambulia kwa kushtukiza mara chache na kupoteza muda.

## Gamondi, Taoussi mechi ya marafiki

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema watapambana na Azam FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, kwa namna ,watakavyokuja'.

Gamondi amesema watawaangalia kwanza Azam jinsi watakavyocheza ili nao wajue namba ya kukabiliana nao na hatimaye kupata ushindi katika mchezo huo.

Kocha huyo alisema kwa sasa timu nyingi zinapokutana na Yanga zinacheza mtindo tofauti, nyingine zikicheza kwa kukamia zaidi, mpira mirefu, ubabe, hivyo yeye atapanga mbinu baada ya kubaini mfumo wao.

"Azam ni timu nzuri na ina wachezaji wazuri mno, wana kocha mzuri kwa hiyo haitakuwa mechi ya kitoto, lakini tunafanya kila kitu kwa ajili ya ushindi, katika soka chochote kinaweza kutokea, kila timu ikija inataka kupambana na sisi kwa njia tofauti, wakati mwingine kuonyesha ubabe, lakini tunapambana kadri ya uwezo wetu, kwa jinsi timu inavyokuja ndiyo tunajua tupambane vipi," alisema Gamondi.

Aliongeza itakuwa furaha kwake kucheza na timu inayofundishwa na ,rafiki' (Rachid Taoussi), ambaye amewahi kufanya naye kazi, hivyo wanafahamiana.

„Nadhani tutakuwa na mchezo mzuri dhidi ya Azam, itakuwa mechi nzuri sana kwangu kwa sababu kocha wa timu hiyo ni rafiki yangu sana, tuliwahi kufanya kazi pamoja, tunafahamiana kwa miaka 25 iliyopita," Gamondi alisema.

Aliisifia Azam ni timu nzuri kutokana na kuundwa na wachezaji wenye viwango vizuri.

Naye Taoussi amesema anapenda sana kucheza michezo migumu kama hiyo.

"Tunakwenda kucheza mechi kubwa, huwa napenda michezo ya aina hii kwa sababu hata sisi Azam ni timu kubwa hapa Tanzania, tuna wachezaji wakubwa, nadhani kama sita hivi wanacheza kwenye kikosi cha timu ya taifa.

Nataka kwenda kushinda mchezo dhidi ya rafiki yangu Gamondi, namfahamu sana na yeye ananifahamu kitambo tu, kifupi tunafahamiana sana," alisema Taoussi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >